ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.

18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.

38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53.Mhe. Asha Bakari Makame	Uteuzi wa Rais.
54. Mhe. Asha Moh’d Hilal	Jimbo la Magogoni.
55.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
58.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
59.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
60.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
61Mhe. Hasnuu Moh’d Haji	Uteuzi wa Rais.
62.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.

63.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
64. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
65.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
66.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
68.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
69.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
70. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
71.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
72.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
73.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
74.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
75.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
76.Mhe. Saleh Ramadhan Feruz	Uteuzi wa Rais.
77.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
78..Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
79.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
80.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Tatu – Tarehe 11 Agosti, 2010

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

Dua

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe kwa furaha na kwa heshima kubwa naomba kuwapa taarifa kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Amani Abeid Karume atalihutubia Baraza la Wawakilishi leo tarehe 11/8/2010 Saa 10.00 Alasiri.

Kwa hivyo nawaomba waheshimiwa wajumbe nyote wa Baraza la Wawakilishi tuhudhurie sote ili tuweze kumsikiliza Mhe. Rais wetu ambae ni sehemu ya Baraza kwa mujibu wa kifungu cha sitini na tatu cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Waheshimiwa Wajumbe nimemualika pia Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar awe nasi wakati wa hotuba hiyo ya Mhe. Rais, hata hivyo Mhe. Jaji Mkuu hayupo nchini kwa hivyo atawakilishwa na jaji namba moja wa Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Vile vile tumewaalika watu mbali mbali mashuhuri wahudhurie kuja kusikiliza hotuba hiyo ya Mhe. Rais wa Zanzibar, kwa ujumla ni kwamba tutakuwa na wageni mbali mbali katika kikao chetu cha jioni ya leo.

Waheshimiwa Wajumbe tunawaomba nyote mfike saa 9.00 Laasiri Mhe. Rais atafika saa tisa na nusu laasiri ambapo atapokea salamu ya heshima na kukagua gwaride lililoandaliwa na Jeshi la Polisi na baadae saa 10.00 jioni ndipo tutaanza na kikao cha Baraza ili Mhe. Rais aweze kutoa hutuba yake.

Waheshimiwa wajumbe hivi punde nitawaomba tufanye utaratibu wa kutuwezesha tukutane saa 10.00 badala ya saa 11.00 kama ilivyo kawaida, vile vile tufanye utaratibu wa kutuwezesha kuwaruhusu anayemuwakilisha Mhe. Jaji Mkuu na ADC wa Mhe. Rais waweze kuingia kwenye ukumbi wa Baraza la Wawakilishi.

Waheshimiwa Wajumbe ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: sasa waheshimiwa wajumbe hii para ya mwisho inataka tufanye kazi mbili, moja ya kuitisha kikao chetu saa 10.00 jioni badala ya saa 11.00 kama ilivyo kawaida na vile vile humu ndani tuwe na wageni maalum ambao wapande huku juu nao ni Mhe. Jaji anayemuwakilisha Mhe. Jaji Mkuu pamoja na Mpambe wa Mhe. Rais. Sasa kwa mnasaba huo namuomba Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi atoe hoja ili kuwezesha utaratibu huo ufanyike.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba utenge kanuni kando ili kumuwezesha Jaji nambari moja kuweza kuingia ukumbini kwa niaba ya Jaji Mkuu.

Pili naomba utenge kanuni kando ili kumuwezesha mpambe wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nae aingie ukumbini katika shughuli yetu ya ufungaji wa Baraza.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri hebu rudia ili tuwe na uhakika hoja ya pili ni kikao kuanza saa 10.00 badala ya saa 11.00 kama ilivyo kawaida, hebu na hii iweke pamoja ili tukamilishe utaratibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja tatu, hoja ya kwanza ni kutoa ruhusa ya kutenga kanuni kando kumuwezesha Jaji ambae atamuwakilisha Jaji Mkuu wa Zanzibar kuweza kuingia katika ukumbi wetu huu.

Pili naomba kutoa hoja ya mpambe wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ADC wake nae aweze kuingia ukumbini.

Mhe. Spika, pia naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu jioni ya leo lianze shughuli zake saa 10.00 badala ya saa 11.00.

Mhe. Spika, zote tatu kwa pamoja naomba kuzitolea hoja.

Mhe. Spika: Wale wanaokubaliana na hoja za Mhe. Waziri wanyanyue mikono, na wanaokataa wanyanyue mikono. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Spika: Kwa hivyo kikao chetu cha leo kitaanza saa 10.00 badala ya saa 11.00 na ruhusa imetolewa Mpambe wa Rais pamoja na Mheshimiwa Jaji anayemuwakilisha Mhe. Jaji Mkuu waingie humu ukumbini kwa ruhusa yenu Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana.

Waheshimiwa wajumbe kikao chetu cha leo asubuhi hii ilikuwa ni kikao cha utaratibu na taratibu hizi tumeshajiwekea lakini ni vizuri baada ya kukaa kwa miaka mitano basi kiongozi wetu wa shughuli za serikali ndani ya Baraza hili angepata nafasi ya kutoa neno la shukurani kwenu, jioni tunategemea atatoa shukurani kwa Mhe. Rais lakini hivi sasa iwe shukurani kwa waheshimiwa wajumbe.

Mhe. Waziri Kiongozi: Bismillahi Rahmani Rahim Mhe. Spika, kwa jina la Mwenyezi Mungu napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru viongozi, watendaji mbali mbali, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kazi nzuri na kubwa ya kupigiwa mfano ambayo wamekuwa wakiifanya takriban kipindi cha miaka 10 iliyopita.

Kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa namna unavyoliongoza Baraza lako tukufu, umekuwa ukiliongoza Baraza letu kwa hekima na busara kubwa kwa hiyo tunakushukuru sana na Mwenyezi Mungu akubariki.

Pili, namshukuru sana ndugu yangu Katibu wa Baraza na watendaji wake wote wa Baraza kwa hatua mbali mbali na huduma ambazo wamekuwa wakizitoa kwetu kwa kipindi chote hicho. Tatu, nawashukuru rafiki zangu wafanyakazi wenzangu wa muda mrefu waandishi wa habari kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuripoti na kutoa taarifa mbali mbali ya shughuli ambazo tumekuwa tukizifanya hapa, maana kama si weledi wao na kazi yao hiyo nzuri, basi sehemu kubwa ya wananchi wasingekuwa wakipata habari na taarifa juu ya shughuli tunazozifanya katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, Zanzibar ina historia ndefu sana, Zanzibar ni miongoni mwa visiwa vyenye historia iliyotukuka na historia ya muda mrefu. Lakini Zanzibar pengine miongoni mwa visiwa vyenye historia hiyo ya muda mrefu, ni miongoni mwa visiwa vichache ambavyo havijaweza kupiga hatua kubwa sana ya maendeleo tunayoyahitaji. Sisi Zanzibar hatuna tofauti sana na historia ya Singapore, Mauritius na kwa bahati mbaya visiwa viwili hivi nilivyovitaja kila walichokuwa nacho wao na sisi hapa Zanzibar tunacho na pengine sisi Mwenyezi Mungu ametubariki zaidi kuliko wao.

Naomba nitaje mifano mitatu. Singapore ni ndogo pengine Singapore mara tatu au mara nne ndio tunaweza tukapata ukubwa wa Zanzibar, Mauritius pengine hatuna tofauti kubwa sana Singapore wana makabila Wahindi na watu wenye asili kutoka China. Mauritius wanao Wahidi, watu wenye asili ya Kiafrika na Wafaransa kidogo. Zanzibar watu wenye asili ya Kiafrika, Kiarabu, watu wenye

asili ya Kihindi eneo la kijografia maeneo yote haya yako kwenye eneo zuri la kijografia ambalo ni muafaka sana kwa biashara na mawasiliano.

Waheshimiwa Wajumbe mtakubaliana na mimi kwamba Zanzibar iko kwenye nafasi nzuri zaidi kuliko mataifa mawili haya niliyoyataja. Kwa hivyo, wataalamu wa maendeleo na siasa wamekuwa wakijiuliza tatizo la Zanzibar ni nini? Pengine tatizo la Zanzibar ni migogoro ya kisiasa ndio ambayo imetuzuia kufika huko tulikotarajia.

Mhe. Spika, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba Wazanzibari wamefikia mahali na wakatanabahi juu ya ukweli huu kwamba Zanzibar ya leo, Zanzibar ya kesho inategemea sana mchango wa kila Mzanzibari wa ndani na nje ya nchi yetu. Haikunishangaza sana mnamo tarehe 9 Julai, 2010 Wajumbe wa Baraza lako tukufu walifanya maamuzi ya kihistoria, maamuzi ambayo ni marekebisho ya Katiba ya 10 ambayo pamoja na mambo mengine yataongeza idadi ya akina mama kutoka asilimia 30 kwenda asilimia 40. Kubwa zaidi ni kuridhia kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Waheshimiwa Wajumbe wenzangu napenda kuchukua nafasi hii kulishukuru sana Baraza lako tukufu kwa hatua kubwa ya kihistoria tuliyoichukua. Najua jambo hili halikuwa jambo rahisi, lakini kwa mwaka huu wa 2010 na katika Baraza hili unaloliongoza jambo hili limewezekana na hatuna budi kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ukarimu na neema yake hiyo aliyotupa.

Mhe. Spika, madhumuni ya kufanya marekebisho haya ya katiba kwanza ni kutafuta umoja na maelewano ili kila Mzanzibari atoe mchango wake katika maendeleo ya taifa letu kwa mujibu wa uwezo na kipaji alichomjaalia Mwenyezi Mungu. Pili kupunguza migogoro ya kisiasa isiyokuwa ya lazima na tatu kushughulikia matatizo ya umasikini yanayowakabili watu wetu.

Mhe. Spika, kwa mnasaba huo basi ili sisi Wazanzibari tuweze kukidhi matarajio ya wananchi wetu katika kufikia nchi yenye matumaini na neema siku zinazokuja. Natamani sana serikali itakayoingia madarakani baada ya uchaguzi wa Oktoba, 31 2010 iwe na watu wenye moyo mkubwa wa uzalendo, iwe na watu walio makini, iwe na watu wenye moyo wa uwajibikaji wa hali ya juu, iwe na watu wenye uwezo wa hali ya juu katika kushughulikia matatizo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, aliyekuwa mwanaharakati wa haki za Umarekani wenye asili ya Kiafrika marehemu Martin Luthar King alisema maneno yafuatayo na naomba uniruhusu niseme kwa lugha yake ya asili, alisema hivi:

"I have a dream that all my four children will one day live in a nation where people will not be judged by the colour of their skin but the content of their character I have a dream".

Martin Luthar King alisema anayo ndoto kwamba siku moja watoto wake wote wanne wataishi katika taifa ambalo watu hawataangaliwa na kuhukumiwa kwa sababu ya rangi ya ngozi yao, bali wataangaliwa kwa tabia zao kwa hulka zao na matendo yao. Na mimi ninayo ndogo kwamba siku zijazo watu wa Zanzibar hawataangaliwa na kuhukumiwa kwa sababu ya maumbile yao, bali watahukumiwa kwa sababu ya uzalendo wao, umakini wao na utumishi wao kwa taifa lao.

Nina matumaini makubwa kwamba serikali itakayoundwa baada ya mwezi oktoba 31 Mwenyezi Mungu akipenda itatekeleza wajibu wa msingi huo, lakini hatuna budi kujua ukweli mmoja kwamba kila mazingira mapya yana matatizo yake na vizuri basi wale watakaopata nafasi kutumikia serikali hiyo kuujua ukweli huu, katika historia za serikali zote za umoja wa kitaifa zenye mnasaba wa serikali hii tunayotarajia kuiunda baada ya uchaguzi.

Mwanzoni kama ilivyo kwa mambo yote duniani mwanzo kidogo unakuwa na misuko suko kidogo kwa sababu watu wanahitaji kufahamiana, lakini hili likitokea lisituvunje moyo tunahitaji kuwa wastahamilivu, tunahitaji kuwa watulivu. Lakini la msingi tuelewe kwamba tunao wajibu mkubwa

sana wa kukidhi matarajio ya Wazanzibari wote sasa matatizo yakijitokeza tusivunjike moyo tutulie na tutafakari twende mbele na tukifanya hivyo nina hakika tutaweza kukidhi matarajio ya Wazanzibari.

Kwa maana hiyo basi namuomba Mwenyezi Mungu aijaalie serikali hiyo iwe na uwezo wa kushughulikia matatizo ya Wazanzibari hasa suala la kushughulikia matatizo ya umasikini, matatizo ya umasikini tuliyokuwa nayo yanaweza kupata dawa muafaka kama kila mmoja wetu atajitahidi kufanya kila linalowezekana kushughulikia matatizo hayo, kwa bahati nzuri kama sisi Chama tawala chini ya uongozi wa Rais katika kipindi cha miaka kumi tumeweza kuyafanya haya tuliyoyafanya pengine tukiwa peke yetu, nina matumaini tukiongeza na nusu ya pili katika serikali ijayo nina hakika kama tulifanikiwa kwa asilimia tisini basi hakuna sababu ya kutuzuia tusifikie mafanikio ya asilimia mia moja. *(Makofi)*

Nalisema hili nikiamini kwamba waswahili wanasema umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu na kwa maana hiyo basi Mhe. Spika, mimi nina matarajio makubwa juu ya mafanikio ya serikali inayokuja.

Baada ya kusema hayo basi Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwatakia kila la kheri, kuwatakia maisha mema waheshimiwa wajumbe wenzangu hawa Mwenyezi Mungu aturudishe sote katika sehemu tunazoishi salama, kwa wale ambao tumebahatika kupita kwenye mchakato wa awali kwenye vyama vyetu na hatimae kufanikiwa penye uhai kuwa wagombea wa vyama vyeti na pengine kushinda katika uchauguzi kwenye majimbo yetu, tutapata nafasi tena ya kurudi hapa na kushirikiana katika kuijenga nchi yetu.

Lakini kwa bahati mbaya wapo wenzetu hawakufanikiwa na kwa maana hiyo hatutapata nafasi kuwa nao, nawaomba wasivunjike moyo kuvunjika kwa koleo sio mwisho wa uhunzi. Mwenyezi Mungu atawajaalia wapate shughuli nyengine za kuzifanya na nawaomba katika sehemu yoyote wayatakayokuwa tuendelee kushirikiana nao katika kujenga na kuimarisha maendeleo ya taifa leo na wao, nawatakia kila la heri katika kazi zao mpya watakazojaaliwa kuzifanya.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nakutakia wewe na familia yako kila la kheri mungu akubariki sana ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri Kiongozi nakushukuru kwa maelezo yako haya ya shukurani juu ya hali halisi ya mwelekeo wa nchi yetu ambao ni mwelekeo mzuri na serikali inayokuja, kama ulivyosema una tamaa sana kwamba itasaidia katika maendeleo ya jamii. Umetuasa kwamba pale patakapotokea matatizo ya hapa na pale basi ustahamilivu ndio njia pekee itakayosaidia, umewashukuru pia waheshimiwa wajumbe kwa kukaa nao kwa muda wa miaka mitano sasa tulishirikiana katika shughuli zetu muhimu ambazo zimekwenda vizuri moja wapo ni shughuli kubwa muhimu ya marekebisho ya kumi ya katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Waziri Kiongozi nasaha zako tumezisikia na mimi nakushukuru sana kwa hotuba hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe kabla na mimi sijatoa shukurani zangu nataka nitoe taarifa kwa iliyo muhimu kwa yale mambo ambayo tulikubaliana kwamba tuyatengeneze, moja ilikuwa ni kujaribu kutengeneza hati ya kumtunuku Mhe. Rais kwa kazi nzuri ambayo amefanya kwa ajili ya nchi yetu na hasa hasa utulivu mkubwa wa kisiasa ambao ameuleta katika nchi hii.

Sasa naomba kutoa taarifa kwamba hati hiyo imetayarishwa na baadhi yetu wawili watatu tumeiona itakuwa na marekebisho kidogo kuliko vile ambavyo tulikuwa tukisema, hati itajieleza kwamba wajumbe walioorodheshwa chini tunamtunuku Mhe. Rais hati ile maalum kwa maendeleo makubwa aliyotuletea nchini kwetu, sasa hiyo hati hatutotia saini kama vile tulivyopanga mwanzo isipokuwa yale majina tu yaliyojieleza wenyewe ya Wajumbe wote wawakilishi kwa umoja wetu tunamtunuku Mhe. Rais.

Utaratibu wa kukabidhi hati hii utafanyika leo humu ndani pale ambapo Mhe. Rais atamaliza hotuba yake na maneno ya shukurani yametoka kwa Mhe. Waziri Kiongozi na Mhe. Kiongozi wa Upinzani, sasa wakati wa shukurani za Spika, basi na hati hiyo itakabidhiwa kwake. Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa hati ambayo tumepitisha wenyewe kwamba tumtunuku Mhe. Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya.

Jengine tulipanga kwamba tutengeneze jiwe ambalo litakuwa na majina ya wajumbe wote jiwe hilo litakuwa ni kumbukumbu ya Baraza hili na Wajumbe wake kwa kufanya kazi moja kubwa sana ya kihistoria ya kuleta mshikamano wa kisiasa na kuleta mfumo mpya wa serikali, mlinituma kwamba nimwambie Sheikh atutengenezee jiwe hilo. Kazi hiyo nimeifanya na amekubali kwamba jiwe hilo atalitengeneza. *(Makofi)*

Kwa hivyo kazi yetu moja iliyobakia ni baadae sisi kama ofisi kumpelekea majina ili aweze kutengeneza jiwe hilo, pamoja na maelezo ambayo tunataka ayaandike pale juu sasa hivyo ndivyo ambavyo imekuwa kwa shughuli zetu mbili tulizoamua hapa ili tuzifanye.

Shughuli ya tatu ilikuwa ni kumuomba Mhe. Rais nae atoe hati hii tutamuarifu na kumuomba afanye hivyo sasa ni juu yake tena kusema sawa au sio sawa, kwetu sisi tutamuomba hivyo kama mlivyoelekeza nyinyi waheshimiwa wajumbe. Kazi hiyo ya kumuandikia Mhe. Rais tutaifanya ofisi kwa niaba yetu ili hatimae Mhe. Rais nae ataamua nini cha kufanya.

Nilitaka nitoe taarifa hizo tatu kuhusiana na hicho nilichozungumza na kukubaliana katika Baraza letu hili.

Waheshimiwa wajumbe nami naomba nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwenu nyote kwa kunisaidia sana kuendesha vikao mbali mbali vya baraza hili, nikisaidiwa na Mhe. Naibu Spika, ambae sasa hivi hayupo mwenzetu Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu hakuweza kuingia kwenye shughuli hizi akiendesha vikao kutokana na hali yake ya afya. Lakini ushauri na baadhi ya mambo ambayo alikuwa anapendekeza tulikuwa tunapeana kiofisi. *(Makofi)*

Nachukua nafasi hii vile vile kuwashukuru Wenyeviti wa Baraza wote ambao kimsingi ndio waliokuwa wakinisaidia kuendesha vikao vya Baraza, nianze kumshukuru sana Mhe. Ali Mzee Ali yeye ndio *senior* Mwenyekiti ambae kwa muda wote amekuwa ananisaidia sana kuendesha vikao hivi, hasa hasa pale ambapo Mwenyekiti mwengine Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi hajachaguliwa. *(Makofi)*

Lakini nichukue nafasi hii vile vile kumshukuru sana Mhe. Thuwaybah Edington Kisassi mara baada ya kuchaguliwa hakuwa akihitaji mafunzo yoyote kuwemo kwake ndani ya Baraza hili amemudu kunisaidia vile vile kuendesha vikao vya Baraza, hapana shaka mtakubaliana nami kwamba Katibu wangu alijitahidi sana kutayarisha kazi za Baraza hili pamoja na kazi nyengine za kiofisi kwa uwazi na mafanikio makubwa. Katibu akishirikiana na watendaji wenzake pia wamekuwa wananishauri mambo mbali mbali hasa yale ambayo yanahusu taratibu pamoja na masuala ya kisheria. *(Makofi).*

Ili kuhakikisha kwamba shughuli zetu zinakwenda kwa mujibu wa taratibu zetu tulizojiwekea na zimekuwa za mafanikio makubwa na wananchi wamekuwa wanapata faida kubwa kwa yale tunayoyaeleza humu ndani na isingekuwa hivyo kama sio kwa msaada mkubwa unaofanywa na wenzetu watu wa habari, ambao kwa muda wote wakati wa vikao tunakuwa nao katika kumbi zetu za Baraza la Wawakilishi. Wenzetu hawa wakati sisi tumekaa wao muda wote utawakuta wamesimama kama hivi wanachukua picha. Lakini na wengine wanachukua habari kiasi cha kwamba tu baada ya kumaliza shughuli yetu taarifa wanachukua pamoja na wananchi wetu kujua kile kinachoendelea katika nyumba yao tukufu hii.

Nachukua nafasi hii kuwashukuru sana ndugu zetu wa ulinzi Polisi na usalama shughuli zetu humu ndani zimekuwa zikiendeshwa bila ya wasi wasi kwa sababu ya ndugu zetu wa polisi ambao mara kwa mara wanahakikisha kwamba usalama upo, lakini pia na wenzetu wa usalama nao wamejitahidi

kufanya kazi nzuri ili kuhakikisha kwamba shughuli zetu zinakwenda vizuri. Nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa kazi yao hiyo njema.

Waheshimiwa wajumbe kikao cha leo asubuhi ni kikao cha utaratibu na kupeana taarifa za mambo mbali mbali, nimesikia kitu kinasema kwamba wabeba rungu ni kweli utaratibu wetu tunapoingia ukumbini humu na kutoka basi wanatuongoza kiutaratibu wa kuingia humu kwa heshima kabisa ni wabeba rungu wetu, wakiongozwa na ndugu Mussa Ali Mtwana pamoja na wenzake wote wamefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Lakini humu ndani huwa tunafanya mawasiliano mbali mbali kwa kuandikiana vi- *note* na mimi wakati mwengine huwa ananiandikia Mhe. Abdalla Mwinyi na Mhe. Mustafa ambavyo ananiandikia na wengine wengi na kazi ya kufikisha ujumbe huo huwa inafanywa na wahudumu wetu humu ndani, naomba nichukue nafasi hii pia niwashukuru sana kwa kazi yao hiyo. *(Makofi).*

Lakini natana nitoe shukurani maalum kwa watumishi wetu mbali mbali kwamba kwa muda wote wamekuwa wakiweka heshima kubwa sana kwa wajumbe, jambo ambalo kwao wao ni lazima wafanye hivyo, wanaweka heshima hiyo bila ya ubaguzi kwamba huyu ni wa Chama Tawala na huyu ni wa Chama cha Upinzani wanatoa heshima hiyo na huduma yao vizuri sana kwa waheshimiwa wajumbe wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa wajumbe nirudie kuwashukuru kwa sababu ya jambo moja kubwa na muhimu, bahati nzuri mimi mwenzenu mmeniweka kwenye kiti hiki hichi ni kipindi cha tatu na naelewa mambo yalivyokuwa huko nyuma kiasi miaka kumi iliyopita, lakini naelewa pia mambo yalivyo hivi sasa na karibu kwa kipindi chote cha miaka mitano, hali huko nyuma ilikuwa ngumu hatukuwa tukisemezana vizuri, hatukuwa tunashirikiana vizuri. Lakini leo hii kwa kweli mazingira yamebadilika sana ndani ya Baraza letu hili. *(Makofi)*

Si rahisi kama si utaratibu wa kukaa kulia na wajumbe wa Chama tawala na kushoto ya Spika ni wajumbe wa upinzani haingekuwa rahisi kujua nani wa upinzani, nani wa Chama tawala, sasa ni utaratibu tu ndio umetufanya kuwa katika hali duni hizi, lakini vyenginevyo mashirikiano imekuwa ni jambo la mfano katika kufanya kazi katika Baraza letu. Jambo hilo limeifanya kazi yangu kuwa rahisi sana kwa hivyo nichukue nafasi yangu maalum kuwashukuru sana waheshimiwa wajumbe kwa vile tunashirikiana pamoja kwa ajili ya kuendesha shughuli zetu.

Maingiliano yetu na mashirikiano yetu imekuwa ni dira sahihi kwa wananchi wetu tuishi je na tufanye vipi katika maisha yetu ya kawaida. Sisi kama viongozi ni kigezo cha wananchi wetu walioko uraiani, tukienda vibaya humu ndani bila ya shaka na wananchi watakwenda kwa hatua zile zile ambazo sisi tunakwenda. Lakini kwa kwenda vizuri hivi ndio maana sasa mitaani utakuta kumetulia sana wala hakuna matatizo yoyote.

Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana sana kwa hilo na kuifanya kazi yangu kuwa nyepesi na kuelekeza wananchi njia ya kupita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe baada ya machache hayo naomba sasa nichukue nafasi hii kuahirisha kikao hiki hadi saa 10.00 jioni, tusisahau tu kwamba kufika kwetu ni saa 9.00 kwa sababu kutakuwa na gwaride la heshima na wajumbe wote tunataka mushuhudie, mara baada ya hapo tuingie ukumbini ili Mhe. Rais aje kutoa hotuba yake.
Kikao kinaahirishwa hadi saa 10.00 jioni.

(Saa 3.45 Asubuhi Baraza liliahirishwa hadi Saa 10.00 jioni)

(Saa 10:00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Amani Abeid Karume, Mhe. Jaji wa Mahakama Kuu Mhe. Mshibe Ali Bakari, Waheshimiwa Wajumbe.

Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais kukubali leo hii kuja kwa ajili ya kazi moja muhimu sana nayo ni kutoa nasaha zake na baadaye akalivunja hili Baraza. Sijui kama mmefurahi.

Lakini kuvunjwa kwa Baraza hili ndio mchakato unaanza rasmi wa kutengeneza Baraza jengine. Kwa hiyo tusiwe na wasi wasi kuvunjika kwa koleo sio mwisho ya uhunzi.

Mhe. Rais kabla ya kuanza shughuli zetu tutakuwa na matukio mawili. Kwanza ni kuwatambua wageni wetu mashuhuri, ambao wapo hapa juu na nitaomba waheshimiwa wajumbe pale ninapomtaja mgeni mmoja mmoja basi tumpongeze kwa kawaida zetu. Na mgeni mwenyewe nitapenda asimame ili wajumbe wageuke kidogo kumuona.

Katika wageni wetu mashuhuri ni mama Shadia Karume, yupo pamoja na mama Shamsi Nahodha, yupo pia mama Shamhuna. Tunaye mstahiki Meya, waheshimiwa mabalozi wadogo mbali mbali waliokuwepo nchini kwa pamoja naomba wanyanyuke. Bila ya kumsahau mama yetu mkuu mama Fatma Karume.

Kwa kuwa Baraza hili leo linavunjwa basi na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi naye amekuja kushuhudia ili atengeneze utaratibu mwengine wa Tume ya Uchaguzi. Mhe. Mwenyekiti, wa Tume ya Uchaguzi naona yupo mbali kidogo lakini na yeye ni mmoja kati ya watu tuliowaalika.

Mhe. Rais naomba niwakaribishe wageni wengine wote tuliokualikeni na mmefika, nakushukuruni sana na huu ndio ukumbi wenu mpya ambao tunafanya shughuli zetu humu.

Mhe. Rais tukio jengine tunataka tukukabidhi hati. Waheshimiwa Wajumbe hawa kwa umoja wetu tumeona ni muhimu na tunatambua kazi yako kubwa uliyoifanya katika nchi hii ya Zanzibar, hasa katika kuleta amani na utulivu kwa njia ya maridhiyano.
Sio hivyo tu Mhe. Rais, pamoja na amani na utulivu ambao wewe Mhe. Rais ndio kinara wa mambo hayo. Lakini pia umeleta maendeleo makubwa sana katika nchi hii. Kuhusiana na suala letu zima la maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa hakuna mtu ambaye hajui kuhusu hili. Inafahamika ndani ya nchi na nje ya nchi kwamba kazi hiyo umeifanya vizuri sana.

Mhe. Rais kwa kutambua kazi yako hiyo kubwa na muhimu uliyowafanyia wananchi wa Zanzibar na nchi yako. Sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumeona na tumetambua kazi hiyo kubwa kwa hiyo tuna furaha leo tukutunuku hati maalum inayothibitisha kazi hiyo kubwa uliyoifanya kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar.

Kwa hiyo naomba ukubali ili nikukabidhi hati hiyo mbele ya wajumbe ili kuthibitisha kile ambacho nilichokizungumza kuridhika na kazi zako nzuri ulizotufanyia wananchi wa Zanzibar. (*Makofi*)

Naomba sasa nikukabidhi hati ambayo Waheshimiwa wajumbe wanakutunukia leo hii tarehe 11/8/2010. (*Makofi*)

Ahsanteni sana. Nimemuona Mhe. Rais ametabasamu, kuthibitisha lile sisi ambalo wenzake tumeamua kumtunuku. Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana.

Mhe. Rais kazi ya leo ni kusikiliza hotuba yako na baadaye ulivunje Baraza. Nakushukuru umekubali kuja kuifanya kazi hiyo na sasa Wajumbe hawa pamoja na wageni wetu mbali mbali waliyokuwepo pale juu wanahamu kabisa na wapo tayari kusikiliza hotuba yako na mwisho uvunje Baraza hili. Mhe. Rais karibu.

HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI, MHE. DR. AMANI ABEID KARUME KUAGANA NA WAHESHIMIWA WAJUMBEWA BARAZA LA WAWAKILISHI LA SABA, TAREHE 11 AGOSTI, 2010

Mhe. Spika,

Mhe. Waziri Kiongozi,

Mhe. Jaji Mkuu,

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi,

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi,
Waheshimiwa Mabalozi wadogo walioko Zanzibar,

Viongozi wa vyama vya siasa,

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

ASSALAAM ALEYKUM,

Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma na Mwenye Uwezo wa kila Jambo, kwa kutupa afya na uzima tukaweza kujumuika hapa leo kwa ajili ya shughuli hii adhimu. Namshukuru pia kutujaalia amani na utulivu ndani ya nchi yetu vinavyotuwezesha kuendesha mambo yetu kwa mafanikio makubwa.

Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kutumia uwezo wangu wa kikatiba kuhutubia Baraza la Wawakilishi la Saba na kutoa tathmini ya utekelezaji wa baadhi ya shughuli za Awamu ya Sita ya Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar, chini ya Uongozi wangu, kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili na wananchi wote kwa jumla.

Hii ndio nafasi yangu ya mwisho kulihutubia Baraza hili nikiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nashukuru sana kupata fursa hii ambayo, pia, nitaitumia kutangaza rasmi kama ulivyoeleza mwenyewe hapo awali kulivunja Baraza hili.

Mhe. Spika, nchi yetu inaendelea na utaratibu tuliojiwekea wa utekelezaji wa demokrasia ya kupokezana uongozi wa nchi kwa njia ya uchaguzi. Awamu ya Sita ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliingia madarakani Novemba, tarehe 8 mwaka 2000 kufuatia Uchaguzi Mkuu uliofanyika. Muda wa katiba na kisheria wa awamu hiyo panapo uhai unamalizika baada ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba 31, mwaka huu.

Mhe. Spika, ni vyema kujikumbusha tunakotoka, tokea mwaka 2000 mpaka hapa tulipo 2010. Kwanza, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa viongozi walionitangulia wa Awamu zilizopita kwa jitihada zao za kuweka misingi mizuri ya maendeleo ya nchi yetu.

Awamu ya Sita iliingia katika wakati ambao nchi yetu ilikuwa imekabiliwa na matatizo ya kisiasa ambayo yalichangia kuleta hali ya mgawanyiko wa wananchi, kuathiri maendeleo ya miundombinu, kuwepo uchumi dhaifu na uhusiano usioridhisha na baadhi ya nchi marafiki.
Takwimu zinaonesha kwamba pato la Taifa kwa mwaka 2000 lilikuwa T.Shs. 190.5 bilioni na pato la wastani la kila mtu lilikuwa T.Shs. 207,987 sawa na US$ 260 kwa mwaka. Ukusanyaji wa mapato ya ndani ya serikali kwa mwaka 2000/2001 ulifikia T.Shs. 38,674 milioni. Huduma za jamii zikiwemo elimu, afya, maji safi na salama haikuwa ya kuridhisha kutokana na kudhoofika kwa

uchumi wetu. Hali ya miundombinu, zikiwemo bandari, barabara na mawasiliamo, pia ilikuwa si ya kuridhisha. Mwaka huo kulikuwepo skuli za msingi na kati 181, sekondari 28, vyuo 3 na vyuo vikuu 2.

Kwa upande wa afya, vituo vya afya vilikuwa 106 kwa Unguja na Pemba na wananchi wetu wengi waliathirika na ugonjwa wa malaria.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Awamu ya Sita haikuridhika hata kidogo na hali hiyo na ikaamua kufuatilia kiini cha matatizo hayo, yaliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na hali mbaya ya siasa, na kuyatafutia ufumbuzi.

Kwa jitihada za pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chama tawala cha CCM na chama cha upinzani CUF, tulifanya mazungumzo ya pamoja na tukafanikiwa kufikia mwafaka wa mwaka 2001. Hatua hiyo ilisaidia kupunguza hali ngumu ya siasa na kuwafanya wawakilishi wa CUF kuingia Baraza la Wawakilishi na Washirika wetu wa Maendeleo kurejesha uhusiano mzuri na sisi.

Hali hiyo ilisaidia kufungua sura mpya katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu, miundombinu na huduma za jamii.

Kwa mfano, katika mwaka 2004, pato la taifa lilipanda na kufikia T.Shs. 344.3 bilioni wakati pato la wastani la mtu lilikuwa T.Shs. 330,764 sawa na US$ 303. Makusanyo ya kodi yaliimarika na kufikia T.Shs. 59,479 milioni. Serikali kwa makusudi ilifanya mageuzi ya uchumi ambayo yaliwezesha ukuaji wa ukusanyaji kodi, kustawi kwa biashara na vianzio vya uchumi kama utalii, mawasiliano, huduma za fedha nakadhalika. Jumla ya watalii 125,522 walitembelea Zanzibar mwaka 2004 ikilinganishwa na 97,165 mwaka 2000. Idadi ya benki iliongezeka kutoka benki 5 mwaka 2000 kufikia 6 mwaka 2004, na maduka ya biashara ya fedha za kigeni kuongezeka kutoka 14 mwaka 2000 hadi kufikia 24 mwaka 2004.

Utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2000-2005 ulitupa mafanikio katika sekta zote. Huduma za jamii zilipata msukumo mkubwa wa maendeleo. Kwa upande wa elimu, mwaka 2004 tulikuwa na skuli za msingi na kati 229, sekondari 49, vyuo 3 na vyuo vikuu 3, kikiwemo Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar - SUZA tulichokifungua mwaka 2001. Idadi ya wanafunzi katika skuli za msingi ilifikia 199,938 mwaka 2004 kutoka 163,113 mwaka 2000; na wanafunzi wa sekondari 61,002 mwaka 2004, kutoka 42,542 mwaka 2000.

Huduma za afya ziliimarika na vituo vya afya viliongezeka kufikia 122 mwaka 2004. Watoto 37,581 walipatiwa chanjo za magonjwa mbali mbali ya watoto.

Upatikanaji wa maji safi na salama uliimarika kutoka asilimia 35 kwa maeneo ya vijijini na asilimia 70 katika maeneo ya mijini Unguja na Pemba mnamo mwaka 2000 hadi asilimia 51 kwa maeneo ya vijijini na asilimia 75 kwa maeneo ya mijini Unguja na Pemba mwaka 2004.

Mhe. Spika, mipango ya uimarishaji miundombinu iliendelea kutekelezwa na ilipofikia mwaka 2004 barabara kadhaa kuu zilijengwa au kufanyiwa matengenezo.

Kuanzia mwaka 2005 hadi 2010 utekelezaji wa mipango yetu ya kazi za maendeleo ulikwenda sambamba na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005-2010 na katika kipindi cha uhai wa Baraza hili, serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali zilizolenga kuimarisha maendeleo ya wananchi.

Kuhusiana na siha, Sera ya Chakula na Lishe iliandaliwa na kuanza kutekelezwa. Lazima tukiri kuwa upatikanaji wa uhakika wa chakula na lishe bora bado ni changamoto kwa sehemu fulani ya jamii yetu. Kwa vile upatikanaji wa maji safi na salama, pia, ni nyenzo muhimu kwa kuhakikisha jamii ina siha njema miaka mitano iliyopita serikali iliendeleza juhudi za kuwafikishia huduma hiyo muhimu wananchi wengi zaidi, mijini na vijijini, Pemba na Unguja.

Mafanikio ya Kiuchumi:

Mhe. Spika, Kama nilivyotangulia kusema, sambamba na juhudi za kumuendeleza Mzanzibari kiafya na kielimu, katika miaka mitano inayomalizika mkazo uliwekwa katika maendeleo ya uchumi. Wataalamu wanasema kuwa hakuna maendeleo pasipo ukuaji wa uchumi. Dira yetu ya Maendeleo ya 2020 imeweka msisitizo maalumu katika mabadiliko ya kiuchumi (*economic transformation*) kutoka uchumi duni unaotegemea kilimo cha asili na kuelekea kwenye uchumi wa kisasa. Dira pia ilisisitiza maeneo matatu makubwa ya kiuchumi. Mosi, Utalii endelevu, pili, Uzalishaji viwandani; na tatu, Kilimo cha kisasa. Ili kutekeleza mahitaji hayo ya Dira ya Maendeleo, na kwa kutambua hali duni ya miundombinu ya kiuchumi, serikali katika kipindi cha 2005 – 2010 iliweka mkazo katika ujenzi wa mazingira mazuri na misingi imara ya kiuchumi. Mafanikio makubwa yamepatikana katika kukuza uchumi ingawa bado kuna baadhi ya changamoto kuelekea mageuzi makubwa ya uchumi kama yanavyotarajiwa chini ya Dira yetu ya 2020.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kukua kwa thamani ya pato la taifa kutoka T.Shs. 394.9 bilioni mwaka 2005 hadi T.Shs. 878.4 bilioni mwaka 2009 kwa kutumia bei za kudumu za mwaka 2001. Kutokana na ukuaji huo, Wastani wa pato la mtu binafsi nao uliongezeka kutoka T.Shs. 368,000 mwaka 2005 sawa na dola za Marekani 227.0 hadi T.Shs. 728,000 sawa dola za Marekani 557.0 Ongezeko hilo ni la kujivunia ingawa wastani wake umeendelea kuathiriwa na kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu nchini petu. Juhudi maalum zinahitajika kudhibiti kasi hii ili kuendana na ukuaji wa uchumi na kuzuia athari kubwa ya mazingira. Kasi hiyo ya ukuaji ingekuwa kubwa zaidi lakini imeathiriwa na misukosuko ya kiuchumi na fedha iliyojitokeza duniani kote.

Mchango wa Kisekta:

Mhe. Spika, kufuatia mageuzi yaliyotarajiwa katika Dira ya Maendeleo ya 2020, mafanikio ya kuridhisha yamepatikana. Sekta ya huduma ndio iliyoongoza katika mchango wa pato la taifa na ukuaji wa uchumi kwa kuchangia wastani wa asilimia 45 ya pato la taifa katika kipindi hicho. Lengo katika Dira 2020 ni kuwa, sekta hii ichukue jukumu kubwa zaidi la uchumi.

Mafanikio makubwa yamepatikana katika kuimarisha Utalii nchini, ikiwa ni mojawapo ya shughuli za kiuchumi iliyopo chini ya sekta hii.

Thamani ya huduma za mahoteli na mikahawa imeongezeka maradufu kutoka T.Shs. 30.6 bilioni mwaka 2005 hadi T.Shs. 63.1 bilioni mwaka 2009. Aidha, idadi ya watalii wanaotembelea nchi yetu nayo imekua kutoka watalii 125,522 hadi 134,954 katika kipindi hicho. Kwa jumla, mwenendo umekuwa wa kuridhisha katika maendeleo ya shughuli za utalii nchini yanaendana na Dira yetu ya Maendeleo.

Mhe. Spika, Sekta ya Viwanda nayo ilitarajiwa kuchukua nafasi kubwa katika kukuza uchumi. Hata hivyo, imejitokeza kuwa hili ni eneo ambalo linahitaji msukumo wa hatua zaidi katika nusu ya pili ya Dira yetu ya Maendeleo. Sekta binafsi katika uwekezaji na uzalishaji viwandani inahitaji kuhamasishwa na kushiriki vizuri zaidi. Katika miaka mitano iliyopita, mchango wa sekta hii kwa Pato la Taifa kwa wastani ulikuwa asilimia 14.1 tu. Kwa hivyo juhudi maalum zinahitajika katika awamu ya pili ya utekelezaji wa Dira ya 2020.

Uwekezaji wa Rasilimali:

Mhe. Spika, moja ya kichocheo kikubwa cha ukuzaji uchumi ni uwekezaji wa rasilimali. Nchi yetu imeshuhudia kasi kubwa ya kuongezeka kwa thamani ya raslimali iliyowekezwa kati ya mwaka 2005 na 2010 kutoka Tsh. 76.2 bilioni mwaka 2005 hadi Tsh. 178.9 bilioni mwaka 2009. Maeneo yote makuu ya uwekezaji yalirikodi mafanikio makubwa yanayofanana. Uwekezaji kwenye ujenzi wa nyumba uliongezeka kwa asilimia 155 kutoka Tsh. 20.8 bilioni mwaka 2005 hadi Tsh. 52.8 bilioni

mwaka 2009. Ujenzi wa nyumba za biashara ndio ulioongoza ndani ya kundi hilo ambapo uwekezaji wake umepanda kutoka Tsh. 13 bilioni hadi Tsh. 32.2 bilioni. Ujenzi wa nyumba za makaazi umeongezeka kutoka Tsh. 4.1 bilioni hadi Tsh. 10.9 bilioni katika kipindi hiki. Ongezeko hilo ni ishara ya kutosha kuwa wananchi wetu wanaendelea kupata makaazi bora mkiwemo nyinyi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Jambo la kufurahisha zaidi ni kuwa ujenzi wa nyumba vijijini umeongezeka kutoka Tsh. 3.6 bilioni mwaka 2005 hadi Tsh. 9.6 bilioni mwaka 2009. Nawapongeza wananchi wote wa Zanzibar kwa muamko wao wa kujijengea maisha na makaazi bora zaidi.

Mhe. Spika, uwekezaji mwengine muhimu kwa uchumi na maendeleo yetu ni katika ununuzi wa mashine na mitambo kwa ajili ya uzalishaji. Baina ya mwaka 2005 na 2009 uwekezaji huo uliongezeka maradufu (kwa asilimia 101) kutoka thamani ya Tsh. 30.5 bilioni mwaka 2005 hadi Tsh. 61.4 bilioni mwaka 2009. Aidha, thamani ya uwekezaji kwenye ardhi, ujenzi wa barabara na madaraja iliongezeka kwa asilimia 155 kutoka Tsh. 23.1 bilioni mwaka 2005 hadi Tsh. 58.9 bilioni mwaka 2009. Kwa jumla tunapaswa kwa pamoja kujivunia ukubwa wa ongezeko la thamani ya uwekezaji katika maeneo hayo matatu na kwa uwiano uliopatikana.

Biashara ya Kimataifa:

Mhe. Spika, uhusiano wa kibiashara na nchi za nje nao una umuhimu mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi ikiwemo uwazi wa biashara (*Trade Openness*) unaopimwa kwa jumla ya thamani ya uingizaji na usafirishaji. Jumla ya thamani ya biashara na nchi za nje ilifikia Tsh. 150.6 bilioni mwaka 2009 kutoka Tsh. 133.4 bilioni mwaka 2005. Hii ni ishara kuwa nchi yetu imeshiriki zaidi katika biashara na nchi za nje katika kipindi hicho.

Kwa upande mwengine kila nchi huweka jitihada katika kuongeza usafirishaji kwa kadri inavyowezekana na kupunguza uagiziaji. Kwa upande wetu, kwa miaka mitano iliyopita wakati thamani ya uingizaji kimsingi haikuongezeka kutoka kiwango cha Tsh. 120.7 bilioni mwaka 2005 na kufikia Tsh. 120.9 bilioni mwaka 2009, usafirishaji nje umeongezeka zaidi ya maradufu kutoka Tsh. 12.7 bilioni mwaka 2005 hadi Tsh. 29.7 bilioni mwaka 2009.

Mwenendo huo mzuri wa biashara umesaidia kupunguza nakisi ya biashara na nchi za nje kutoka Tsh. 108 bilioni hadi Tsh. 91.1 bilioni baina ya mwaka 2005 na 2009. Aidha, Serikali, pia, imekamilisha uandaaji wa Mkakati wa Usafirishaji (*Zanzibar Export Strategy*) ambao utekelezaji wake unatarajiwa kuimarisha zaidi usafirishaji wa bidhaa kutoka nchini kwetu na hivyo kuimarisha urari wa biashara. Hatua hiyo ni ya kupongezwa na kuimarishwa.

Ukusanyaji wa Mapato:

Mhe. Spika, ili serikali iweze kuhudumia mipango yake yote ya kuleta ustawi mzuri na maendeleo ya wananchi, ilihitaji pia, kuongeza uwezo wake wa mapato. Serikali ilihitaji kusimamia vyema vianzio vilivyopo na kubuni vianzio vipya pamoja na kuangalia mfumo na uwezo wa kitaasisi na kisheria, ili uendane na nia yake ya kujitegemea. Nina furaha kutamka kwamba kwa jumla tumefanikiwa sana katika kuinua uwezo wa serikali kimapato katika kipindi chote cha Awamu ya Sita.

Kama ilivyo kwa maeneo mengine, mapato ya ndani yameongezeka kwa kiasi kikubwa katika kipindi hicho. Mwaka 2005/06 serikali ilikusanya jumla ya Tsh. 68.5 bilioni kutokana na vyanzo vya ndani kupitia Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*) na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (*TRA*). Mwaka 2009/10 taasisi hizi zilikusanya jumla ya Tsh. 146.2 bilioni. Ongezeko hilo la mapato ni sawa na ukuaji wa asilimia 113. Takwimu hizi zinamaanisha kuwa mapato yetu ya ndani yamekua kutoka wastani wa Tsh. 5.7 bilioni kwa mwezi mwaka 2005/06 hadi kufikia Tsh. 12.2 bilioni kwa mwezi mwaka 2009/2010.

Kwa upande mmoja, mafanikio haya ni matokeo ya juhudi za serikali za kuimarisha uchumi kutokana na utekelezaji wa sera za uwekezaji. Kuimarika huko kwa uchumi kumesaidia kuongeza pia wigo wa mapato. Tunamaliza muda wa uongozi wetu tukifurahia mafanikio haya na hasa kuweza kubadilisha

utegemezi wa mapato yetu kutoka yanayotegemea biashara ya kimataifa na forodha na kuwa yanayotegemea zaidi vianzio vyetu vya ndani. Huu ni msingi muhimu wa kuhakikisha kuwa mapato yetu yanakuwa endelevu.

Kwa upande mwengine, mafanikio haya ni matokeo ya kuimarika kwa utendaji wa *ZRB* na *TRA*. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza viongozi na watendaji wote wa *ZRB* na *TRA* kwa juhudi zao. Sehemu ya juhudi zetu za kurekebisha sheria pia, zimechangia katika mafanikio haya. Zaidi ya hayo, tumesimamia vyema pale palipokuwa na dalili za udokozi. Haya yote yamewezekana kutokana na ushirikiano wa pamoja baina ya Serikali na Kamati ya Kudumu ya Uchumi na Fedha ya Baraza la Wawakilishi. Hatuna budi kwa pamoja kujivunia mafanikio haya makubwa.

Usimamizi wa Fedha Za Umma:

Mhe. Spika, ukusanyaji wa mapato pekee bila usimamizi bora wa matumizi ya serikali hauwezi kuleta maendeleo ya wananchi. Kwa kutambua hili, serikali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita iliendelea kuimarisha usimamizi wa fedha za umma. Mfumo wa sheria uliimarishwa kwa kutungwa Sheria mpya ya Fedha na ile ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Serikali hapo mwaka 2005. Utekelezaji wa sheria hizo na Kanuni zake umefanyika katika kipindi cha miaka mitano hii inayomalizika. Serikali, pia, imechukua hatua maalumu za kujenga uwezo wa wahasibu na kuimarisha huduma za uhasibu serikalini. Aidha, kwa kutambua fursa muhimu ya kuimarisha usimamizi kupitia matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano, tumeanza kutumia mfumo wa Kompyuta (*Integrated Financial Management System - IFMS*) unaounganisha Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (Hazina) na Wahasibu Wakuu wote wa Wizara na Taasisi zinazojitegemea, Unguja na Pemba. Mfumo huu umesaidia kuongeza udhibiti, kuimarisha ufanisi, na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za fedha za serikali. Hali hii imesaidia kuwezesha ulipaji wa mishahara ya wafanyakazi serikalini kwa wakati.

Itakumbukwa kuwa moja kati ya kilio kikubwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili na wananchi kwa jumla ilikuwa ni ucheleweshaji mkubwa wa mafao ya wastaafu, yakiwemo kiinua mgongo na pencheni. Serikali ilikuwa inakerwa na tatizo hili. Katika kipindi cha miaka mitano inayomalizika, kufuatia kuimarika kwa hali ya fedha serikalini, juhudi ziliongezwa kulipa deni la wastaafu lililokuwepo na kuhakikisha kuwa malimbikizo mapya yanaepukwa. Serikali imefanikiwa kulipa deni lote la wastaafu hao na kuendelea kulipa wastaafu wapya mafao yao kwa wakati kadri taratibu zinapokamilika. Pamoja na Wajumbe wa Baraza lako, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati watendaji wa Wizara yetu ya Fedha na Uchumi kwa utendaji wao mahiri katika kipindi hicho chote.

Mfumko wa Bei:

Mhe. Spika, maendeleo ya uchumi yanahitaji utulivu wa bei za bidhaa, bei za huduma na thamani ya sarafu. Mfumko mkubwa wa bei, unaathiri imani ya wawekezaji, unapoteza thamani ya sarafu na unaathiri kipato cha wananchi wenye kipato cha kudumu kama vile wastaafu wanaoishi kwa pencheni. Serikali imechukua juhudi kubwa kudhibiti mfumko wa bei katika kipindi cha miaka mitano inayomalizika. Hata hivyo, lazima nikiri kuwa pamoja na juhudi mbalimbali zilizochukuliwa, kasi ya mfumko wa bei imekuwa ya juu kuliko ilivyotarajiwa. Mfumko wa bei kwa mwaka 2005 ulikuwa wa asilimia 9.7, mwaka 2006 asilimia 11.4, na kupanda hadi kufikia asilimia 20.6 mwaka 2008. Sababu ya kasi hiyo kubwa ya Mfumko wa bei imeendelea kuwa ni utegemezi wetu wa chakula tunachoagiza kutoka nje ya nchi hasa mchele, mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia, na kwa kipindi hicho, ujenzi wa bandari ya Malindi ambayo ndio mlango mkuu wa uingizaji na usafirishaji wa bidhaa nchini.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri hali hiyo ilitengemaa mwaka 2009, na bei za chakula na zile za mafuta katika soko la dunia zilishuka. Kushuka huko kulisaidia kupunguza kasi ya mfumko wa bei kutoka asilimia 20.6 ya mwaka 2008 hadi asilimia 8.9 mwaka 2009. Katika kipindi cha kupanda sana kwa kasi ya mfumko wa bei, serikali ilitumia mchanganyiko wa sera zake za mapato (*fiscal policies*),

juhudi za kuimarisha uzalishaji wa ndani wa mazao ya chakula na kuharakisha ukamilishaji wa ujenzi wa bandari ya Malindi ili kupunguza athari ya mfumko huo. Kwa upande wa sera za mapato, serikali ilitoa unafuu maalum wa kodi za uingizaji kama ushuru wa forodha na kodi ya ongezeko la thamani kwa bidhaa za vyakula muhimu zinazoingia nchini. Serikali ilibidi kusamehe mapato yake ilimradi makali ya maisha kwa mwananchi yadhibitiwe.

Ni muhimu kutambua kuwa njia hizo zote ni za muda tu. Ili kudhibiti mfumko wa bei kwa muda mrefu, tunahitaji kuimarisha uzalishaji wa ndani wa chakula na kuimarisha kipato cha mwananchi ili kupunguza sehemu ya pato linalotumiwa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya chakula. Lengo ni kupunguza mchango wa bei za chakula hasa mchele katika faharisi ya bei (*Consumer Price Index*). Aidha, tunapswa pia kuendelea kufuatilia mwenendo wa ujazi (*Liquidity*) wa fedha nchini ili kuudhibiti bila ya kuathiri juhudi za maendeleo na hili pia ni eneo muhimu ambalo lazima tuliangalie.

Huduma za Fedha:

Mhe. Spika, maendeleo ya huduma za fedha ni ishara ya maendeleo ya nchi. Sekta ya huduma za fedha inajumuisha huduma za benki, maduka ya fedha za kigeni, vyama vya kuweka na kukopa na mifuko ya huduma za mikopo midogo midogo. Sekta hii, pia, hujumuisha na huduma za Bima, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na soko la mitaji. Katika kipindi hiki, huduma za benki zimekuwa sana hapa Zanzibar. Mwaka 2005 tulikuwa na Benki sita zilizokuwa zikitoa huduma na hivi sasa zimeongezeka na kufikia Benki kumi. Ongezeko hilo la benki limepelekea mchango wa huduma za kibenki katika Pato la Taifa kuongezeka kutoka asilimia 7.8 mwaka 2005 hadi asilimia 15.3 mwaka 2009.

Miongoni mwa mafanikio makubwa na ya kujivunia zaidi katika eneo hili ni yale ya kuigeuza na kuiimarisha Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ). Mwaka 2000, wakati tunaingia madarakani, PBZ haikuwa na mtaji; ilikuwa ikipata hasara mwaka hadi mwaka na haikuwa na matumaini. Hivi sasa hali imebadilika; tulitumia awamu ya kwanza ya miaka mitano kuiimarisha (*Stabilize*) benki hiyo na miaka mitano inayomalizika kuigeuza kimuundo, kiutumishi, na kimtaji. Maamuzi mengine yalikuwa magumu lakini yalipaswa kufanyika, mfano ni kupunguza idadi ya wafanyakazi; uamuzi ambao ulikuwa na athari kijamii lakini ulikuwa wa lazima.

Tulihimili, pia, msukumo mkubwa wa kuibinafsisha PBZ kutokana na ushauri wa Benki ya Dunia na Benki Kuu ya Tanzania. Wataalam wao hawakutufahamu tulipoamua kutoibinafsisha benki yetu. Kwa hivyo, tulishirikiana kwa pamoja kuimarisha Benki yetu na hivi leo PBZ ina mtaji maradufu ya kiwango cha chini kinachotakiwa na msimamizi wa mabenki yaani Benki Kuu sisi tumeshakivuka. Wakati tunaingia mwaka 2006, PBZ haikuweza kutimiza mtaji wa Tsh. 5.0 bilioni unaohitajiwa na Benki Kuu, leo hii mtaji wa PBZ ni zaidi ya Tsh. 11 bilioni.

Kutokana na hatua madhubuti tulizochukua, tumeweza kubadilisha kabisa muundo wa mtaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar, kutoka benki iliyokuwa ikipata hasara kila mwaka, hadi benki yenye kupata faida kwa mwaka wa nne mfululizo na ilipofika mwezi huu wa Agosti 2010, kwa mara ya kwanza katika historia yake, PBZ imeweza kutoa gawio la jumla ya Tsh. 300 milioni kwa mmiliki wake, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hatuna budi tujipongeze kwa mafanikio hayo.

Miundombinu:

Mhe. Spika, maendeleo niliyoyataja ya mwananchi na uchumi hayawezi kupatikana bila ya kuwepo kwa miundombinu bora. Sehemu za kuingilia na kutokea nchini kama vile bandari na viwanja vya ndege, mtandao bora wa barabara, upatikanaji wa uhakika na wa bei nafuu wa nishati na mtandao bora wa mawasiliano ni nyenzo za msingi kwa nchi kupiga hatua katika maendeleo. Wakati tunaingia madarakani, nchi yetu ilikua na hali duni sana ya miundombinu yote hii. Kwa sababu hiyo, katika kipindi cha uongozi wetu, tulichukuwa jukumu la kuiimarisha miundombinu hiyo ili kushajiisha na kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Naomba sasa nigusie baadhi tu ya mafanikio yaliyopatikana katika maeneo hayo hapa nchini katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Mawasiliano na Uchukuzi:

Mhe. Spika, nchi yetu ni visiwa na sehemu za kuingilia na kutokea za bandari na viwanja vya ndege zina umuhimu mkubwa sana. Kutokana na matatizo ya ujenzi, Bandari kuu ya Malindi ilikuwa katika hali mbaya sana mwanzoni mwa miaka ya 2000. Ushauri wa kitaalam ulionesha kuwa pengine Bandari hiyo isingeweza kutumika tena baada ya mwezi Juni mwaka 2001. Matengenezo yake, kwa hivyo, yalikuwa ni jambo la lazima. Serikali imefanikiwa kuijenga upya Bandari hiyo kwa msaada wa Jumuiya ya Ulaya na fedha kutoka SMZ. Bandari za Mkoani, Wesha na Wete huko Pemba nazo zimeimarishwa.

Kwa upande wa viwanja vya ndege, Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Zanzibar ambao kwa sasa unajulikana kwa jina la "Abeid Karume International Airport" nao umefanyiwa matengenezo makubwa yakiwemo ya kuijenga upya njia ya kutua na kurukia ndege tuliyoizindua siku chache zilizopita pamoja na kuiongeza urefu kutoka mita 2,600 za awali hadi mita 3,022 hivi sasa na hivyo kuwezesha ndege kubwa zaidi za aina zote duniani kutua na kuruka. Hatua hii itasaidia sana katika kukuza usafiri wa ndege pamoja na utalii nchini.

Eneo jengine muhimu na lililokuwa likilalamikiwa sana na wahusika mbalimbali ni udogo wa jengo la abiria katika kiwanja hicho, lakini kwa bahati nzuri tatizo hilo tumeshalipatia ufumbuzi. Na hivi sasa Mkandarasi, Kampuni ya *Beijing Construction Engineering Group Company Limited"* kutoka China inakusanya zana tayari kuanza ujenzi wa jengo jipya na la kisasa katika kiwanja hicho. Ujenzi huo utachukua miezi 36 na unagharamiwa kwa mkopo nafuu wa Serikali ya China kupitia Benki yake ya Exim. Juhudi za kukiimarisha Kiwanja cha Karume Pemba kupitia mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika chini ya miradi ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki nazo zinaendelea. Mawasiliano, pia, yanaendelea baina ya Serikali na Benki ya Dunia juu ya uendelezaji wa kiwanja hicho cha Karume Pemba.

Barabara:

Mhe. Spika, ni jambo la kushukuru na kufurahia kuwa katika Awamu ya Sita nchi yetu imepata maendeleo makubwa katika ustawishaji wa miundombinu ya barabara. Wenyeji na wageni wanaotutembelea leo wanafarajika kwa hali bora ya barabara zetu Unguja na Pemba.

Nakumbusha tu kwamba mwaka 2000, Zanzibar ilikuwa na jumla ya kilomita 447 za lami. Unguja km. 323.5 na Pemba km. 123.5. Kuanzia mwaka huo mpaka mwaka 2009 tumeongeza barabara za lami za km. 753 kuzifanya zote kufikia km. 1,210. Hii ni sawa na asilimia 70.6 za mtandao wote wa barabara Unguja na Pemba.
Leo wananchi wa Donge na Mkokotoni wamefarajika kwa kujengewa barabara yao kwa kiwango cha lami. Hivyo hivyo, kwa wananchi wa Nungwi na wale wa ukanda wote wa utalii wa Matemwe, Pwani Mchangani, Kiwengwa, hadi Pongwe. Hali ndio hiyo, pia, kwa wananchi wa Michamvi, Jambiani, Makunduchi, Kizimkazi, Fumba, Machui, Ghana, na kwengineko. Barabara zote hizi zimesaidia sana sio tu kuwarahisishia wananchi wa maeneo hayo usafiri wao na bidhaa zao, bali pia, zimekuwa chachu katika kukuza maendeleo ya kilimo na utalii endelevu.

Kwa upande wa Pemba, miundombinu ya barabara nayo imeimarika kwa kiasi kikubwa. Kazi ya ujenzi wa barabara za Wete – Konde na Wete – Gando, kwa sababu barabara ya Wete – Gando nisingeiwacha maana kuna rafiki zangu kule kila siku walikuwa wananihimiza. Pamoja na barabara sita za kusini Pemba inaendelea kama ilivyo kwa barabara za Mfenesini - Bumbwini na Amani – Dunga hapa Unguja. Barabara ya Bahanasa Mtambwe nayo iko katika hatua za matayarisho ya ujenzi. Ikifika mwezi wa Novemba mwaka huu, nitakabidhi uongozi wa nchi yetu kwa Rais ajae pamoja na kazi inayoendelea ya uwekaji au ya uwekaji wa miundombinu mbali mbali ya barabara.

Mawasiliano ya Simu:

Mhe. Spika, kutokana na maendeleo ya haraka yanayojitokeza katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, mawasiliano ya simu na huduma zake yameimarika sana kwetu. Jumla ya kampuni tano za mawasiliano ya simu zinatoa huduma hapa Zanzibar ambapo hivi sasa zaidi ya watu 500,000 wanamiliki simu na wengine wana mbili mbili. Mchango wa shughuli za mawasiliano na uchukuzi katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 8.0 mwaka 2005 hadi asilimia 11.0 mwaka 2009, ambapo thamani ya huduma za shughuli hizo imeongezeka kutoka shilingis. 31.5 bilioni mwaka 2005 hadi shilingi 96.8 bilioni mwaka 2009.

Ilikuwa nia ya serikali yetu kuweka njia mpya kuu ya mawasiliano ya habari kwa kutumia *fibre optic cable,* ambao utazunguka visiwa vyote viwili. Lakini pia utaunganishwa na Tanzania Bara na dunia kupitia njia za aina hiyo yenye ufanisi mkubwa wa mawasiliano lakini pia gharama nafuu. Kwa bahati mbaya, maombi yetu ya mkopo nafuu katika Benki ya *Exim* ya China kwa utekelezaji wa mradi huu yalichelewa kupata idhini. Hata hivyo, kwa sasa hatua kubwa imefikiwa na matarajio ni kuwa mradi huu utaidhinishwa kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa 2010. Ukikamilika, mradi pia utasaidia sana kuimarisha ufanisi serikalini kwa kutumia utaratibu wa *e-government*. Mradi pia unatarajiwa kuwa chanzo kipya na umuhimu wa mapato ya serikali. Kwa bahati nzuri sasa, kwa ndugu zetu wa Pemba tayari tumeshaunganisha na njia kuu ya mawasiliano kupitia chini ya bahari kwa kutumia waya wa kupelekea umeme kutoka Tanga. Ndugu zetu wa Unguja itabidi tusubiri kidogo mpaka mradi wa MCC wa waya wa umeme mpya utakapokamilika.

Nishati:

Mhe. Spika, kwa nchi yetu, nishati inajumuisha huduma za umeme, gesi, petroli, kuni na makaa. Katika miaka mitano inayomalizika tumepata mafanikio makubwa ya usambazaji wa nishati ya umeme, lakini pia, tumepata mitihani mikubwa. Mafanikio ni pamoja na kuweza kusambaza umeme katika maeneo mengi zaidi vijijini. Fursa za upatikanaji wa umeme zilizofikiwa hapa Zanzibar ni za kiwango cha juu sana ikilinganishwa na hali iliyopo katika nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara. Hivi karibuni wananchi watakaofaidika na umeme wa uhakika itafikia asilimia 90 ikilinganishwa na asilimia 10 na 15 kwa mataifa mengine ya Afrika Mashariki na Kati.

Mhe. Spika, katika historia yake yote, Pemba ilikuwa haijapata umeme wa uhakika, ilikuwa ikitegemea umeme wa majenereta usioaminika na uzalishaji wake ulikuwa ni wa gharama kubwa. Mwaka 2005 tuliahidi kukiunganisha kisiwa cha Pemba kama ilivyo kwa Unguja, mtandao wa Gridi ya Taifa, kwa vile sasa teknolojia ya kufanya hivyo ipo duniani na tayari tumeshaiona. Tunamaliza muda wetu wa uongozi kwa fakhari kubwa kwa kumudu kuitekeleza ahadi ya kuwapatia umeme wa uhakika wananchi wa Pemba. Kwa maana rafiki zangu wa Gando wale ilikuwa hawaniamini kila nikiwambia tutaunganisha umeme. Wanasema aa umeshatwambia barabara bado na umeme hauji. Lakini leo nashukuru *Alhamdulillah.*

Sasa ni matumaini yangu kuwa, Pemba sasa itapiga hatua za haraka zaidi za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Naomba niwashukuru kwa mara nyengine tena wananchi wote wa Pemba kwa ustahamilivu wao muda wote kabla ya kupatikana kwa huduma hiyo kwa uhakika. Naomba wajue kuwa nathamini sana uvumilivu wao huo na imani yao kwangu. Kwa niaba ya wananchi wote wa Zanzibar, naishukuru tena Serikali na wananchi wa Norway na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msaada wao uliofanikisha mradi huo. Aidha, naishukuru Serikali ya Mapinduzi na wananchi wote wa Zanzibar kwa mchango mkubwa uliokamilisha utekelezaji wa mradi huo.

Mhe. Spika, kwa upande wa Unguja tarehe 29 Julai mwaka 2010 itakumbukwa kuwa ni siku nyengine muhimu kwa historia ya nchi yetu kuhusiana na nishati ya umeme. Siku hiyo tulizindua upya mradi wa majenereta ya akiba Mtoni hapa Zanzibar. Majenereta hayo yana uwezo wa kuzalisha Megawati 25 za nishati ya umeme. Na Waswahili wamesema "***baada ya dhiki faraja***" na pia *"**mvumilivu hula mbivu"***. Vipindi vya kuzimika umeme kwa mwezi mmoja baina ya Mei 21 na Juni 18 mwaka 2008 na baadae miezi mitatu baina ya Disemba 10, 2009 na Machi 8 mwaka huu vilikuwa vipindi vya dhiki sana kwetu sote. Naomba niwashukuru sana wananchi wa Zanzibar kwa utulivu na ustahamilivu wao katika vipindi hivyo vya shida.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kuvuka salama. Aidha, naomba nitambue na kuzishukuru nchi za Norway, Sweden, na Uingereza kwa msaada wao uliotuwezesha kununua majenereta hayo mapya. Kwa utaratibu ule ule wa "abebwae hujikaza". Serikali ya Mapinduzi Zanzibar nayo imetoa mchango mkubwa katika mradi huo. Kupitia kwenu nawapongeza wananchi wote wa Zanzibar kwa mchango wao.

Mafanikio mengine muhimu katika upatikanaji wa nishati ya umeme, ni makubaliano yaliofikiwa na Serikali ya Marekani kwa kutusaidia kuweka waya mpya wa umeme na wenye uwezo mkubwa zaidi kati ya Ras Kiromoni, Dar es Salaam hadi Ras Fumba hapa Unguja. Mradi huu uko katika hatua za utekelezaji, ambapo matengenezo ya waya huo yanaendelea. Tutaikabidhi awamu ijayo ya serikali yetu mradi huo mwengine muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Naishukuru sana Serikali ya Marekani kwa msaada wake huo kupitia Shirika lake la Changamoto za Milenia (*MCC*).

Maendeleo ya Sekta ya Kilimo:

Mhe. Spika, kilimo bado kinaendelea kuwa ni sekta muhimu kwa maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii. Inakadiriwa asilimia 70 ya wananchi wa Zanzibar hutegemea sekta ya kilimo katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Kwa miaka yote serikali imehakikisha kuwa huduma muhimu kwa maendeleo ya sekta ya kilimo zinapatikana kwa wakati. Huduma hizo ni pamoja na matrekta, mbolea, mbegu bora, miche, dawa za kuzuia wadudu waharibifu wa mimea na mazao, dawa za kuzuia magugu, huduma za masoko, umwagiliaji wa maji na ushauri kwa wakulima. Mafunzo maalum kwa wakulima yameendelea kutolewa kwenye maeneo yao, kwenye kituo cha Kizimbani na kwa njia za "shamba darasa". Aidha, tumefanikiwa kuzalisha mbegu bora za mazao mbali mbali na kuzisambaza kwa wakulima wetu ili waongeze tija. Tunalishukuru Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (*FAO*) kwa msaada na ushirikiano wake katika shughuli hizi.

Kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji maji, mnamo mwaka 2001-2003, Shirika la *Japan International Cooperation Agency (JICA)*" kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, walifanya utafiti unaojulikana kama Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji (*Zanzibar Irrigation Master Plan – ZIMP*). Lengo la utafiti huo ilikuwa ni kuangalia uwezekano wa Zanzibar kuweza kulima kwa njia ya umwagiliaji maji kilimo ambacho kina uhakika zaidi. Baada ya utafiti huo wataalamu waliweza kugundua kwamba, Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba ina Hekta 8,521 ambazo zikifanyiwa kazi zinaweza kuendelezwa kwa njia ya kilimo cha umwagiliaji. Eneo hilo linajumuisha mabonde 57 yakiwemo 38 ya Pemba na 19 ya Unguja.
Baada ya kukamilika kwa mpango huo, serikali kwa upande mwengine imefanikiwa kufufua miundombinu ya umwagiliaji maji kwenye eneo la Hekta 740 linalojumuisha mabonde ya Bumbwisudi, Mtwango, Kibokwa na Cheju. Mradi wa Bumbwisudi na Kibokwa ulichangiwa kwa msaada wa Serikali ya Korea Kusini. Pia, kwa kutumia fedha zetu wenyewe, tumefanikiwa kusambaza umeme kwa ajili ya matumizi ya pampu za maji katika maeneo ya Cheju, Bumbwisudi na Kibokwa kwa Unguja na Tibirinzi kwa upande wa Pemba. Aidha, maandalizi ya kusambaza umeme katika mabonde ya Saninga kisiwani Pemba tayari yameshakamilika.

Katika kukamilisha Mpango Mkuu huo wa Umwagiliaji Maji, serikali yetu ikishirikiana na Serikali ya Korea Kusini, hivi karibuni itaanza upembuzi yakinifu katika eneo lilotengwa kwa madhumuni hayo kufuatia kupatikana kwa US$ 1.5 milioni za kazi hiyo. Matarajio ni kwamba, mara baada ya kumalizika upembuzi huo, serikali itapatiwa mkopo nafuu wa kuweka miundombinu katika eneo lote lilobakia la mradi huo. Hatua zote hizo ni muhimu katika suala zima la kujitosheleza kwa chakula hasa mchele.

Aidha, katika kuongeza juhudi za kilimo cha kisasa, serikali yetu imefanikiwa kununua matrekta makubwa 40, matrekta madogo (*power tillers)* 40 pamoja na majembe na zana zake. Aidha, kupitia mradi wa *MACEMP*, serikali imeweza kutunza na kuhifadhi mazingira ya ukanda wa bahari na kuwapatia wavuvi vifaa mbali mbali vyenye thamani ya shilingi 4.8 bilioni.

Mhe. Spika, kutokana na juhudi mbali mbali za kuimarisha uzalishaji, thamani ya bidhaa zilizotokana na kilimo mazao, misitu na uvuvi imeongezeka kwa asilimia 192.9 kutoka thamani ya shilingi 92.5 bilioni mwaka 2005 hadi shilingi 271.0 bilioni mwaka 2009. Kati ya ongezeko hilo thamani ya mazao ya kilimo imepanda kwa asilimia 253.7 kutoka shilingi 51.7 bilioni mwaka 2005 hadi shilingi 182.9 bilioni mwaka 2009.

Thamani ya mazao ya mifugo imeongezeka kwa asilimia 141.1 kutoka shilingi 16.3 bilioni mwaka 2005 hadi shilingi 39.3 bilioni mwaka 2009, ambapo mazao ya misitu thamani yake imeongezeka kwa asilimia 115.4 kutoka shilingi 1.3 bilioni mwaka 2005 hadi shilingi 2.8 bilioni mwaka 2009. Halikadhalika mazao ya uvuvi nayo thamani yake imepanda kwa asilimia 97.4 kutoka shilingi 23.3 bilioni hadi shilingi 46.0 bilioni mwaka 2009.

Ustawi wa Jamii:

Mhe. Spika, sasa naomba kuzungumzia hatua tulizozichukua kustawisha maisha ya wananchi kwa kukuza huduma za jamii kama afya, elimu, maji safi na salama.

Afya:

Pamoja na juhudi zinazochukuliwa katika kuimarisha sekta ya afya kupitia chakula bora na lishe na utumiaji wa maji safi na salama, huduma bora za afya nazo zina umuhimu wa pekee. Katika miaka mitano iliyopita, serikali ilichukua juhudi maalum kuimarisha huduma za kinga na tiba katika hospitali zake Pemba na Unguja. Vituo vya afya vimeongezeka kutoka 141 mwaka 2005 hadi vituo 167 mwaka 2009. Miongoni mwa mafanikio katika sekta ya afya ni ununuzi wa vifaa vya uchunguzi na tiba. Kati ya vifaa hivyo ni mashine za kisasa za uchunguzi, *CT Scan na Fluroscopy, X-ray machines* 3 (2 Pemba na 1 Unguja), *Ultrasound machine*s 2 (1 Unguja na 1 Pemba), *Image intensifier*, pamoja na mashine ya kuchunguza maradhi ya moyo (*Echocardiogram*) na *X-ray* ya meno.

Aidha, serikali imo katika hatua ya mwisho za uwekaji wa "*lift*" mpya kwa hospitali ya Mnazi Mmoja. Lakini pia tayari tumeshanunua mashine za kutolea dawa za usingizi 3, (1 kwa ajili ya Pemba), viti 6 vya kisasa vya kutolea huduma za meno na vifaa vya kufanyia upasuaji.

Katika kipindi hiki, serikali imeifanyia ukarabati hospitali ya macho na kuiwekea vifaa vipya vya uchunguzi na tiba vyenye thamani ya US$ 200,000.

Idadi ya madaktari, wasaidizi wa madaktari na wauguzi iliongezeka kutoka 806 mwaka 2005 na kufikia hadi 859 mwaka 2009. Katika kipindi hicho, tuliendelea kupata msaada wa madaktari wa kigeni kutoka 11 mwaka 2005 hadi madaktari 48 mwaka 2009.

Kwa kushirikiana na Shirika la *Neurosurgical Education Development* la Spain (*NED*), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imefanya operesheni kubwa za kichwa na uti wa mgongo zaidi ya 104 kwa mara ya kwanza katika historia ya Zanzibar. Kabla ya kuwa na *CT Scan* pale na msaada kutoka kwa madaktari hawa wa Spain, huduma hii ya afya ilibidi tuitafute India na kwengineko. Kwa kiasi kikubwa hili liliwezekana baada ya kununuliwa mashine ya *CT Scan.*

Katika jitihada za kujitosheleza kwa madaktari, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa msaada wa Serikali ya Cuba imeanzisha kwa mafanikio mazuri chuo cha udaktari hapa Zanzibar. Sisi wenyewe tumeamua kukiita *Zanzibar Medical School*, kwani kuna ubaya gani si wanafunzi wa udaktari. Hadi sasa wapo wanafunzi 37 Unguja na 12 Pemba. Hawa wanafunzi 37 waliopo Unguja walianza zamani na wanatarajia kumaliza mafunzo yao katika kipindi cha mwaka 2014 baada ya miaka minne tu wata-*graduate* kuwa madaktari kamili.

Kutokana na kuimarika kwa huduma za afya nchini pamoja na mwamko wa wananchi, idadi ya wagonjwa waliopatiwa huduma za tiba iliongezeka kutoka watu 223,351 (2006) hadi watu 348,805 mwaka 2009. Pamoja na kuwa malaria iliendelea kuathiri afya za wananchi, hata hivyo, kutokana na juhudi zilizochukuliwa, serikali imefanikiwa kupunguza malaria kwa kiwango cha kupigiwa mfano.

Kwa sasa, kiwango cha maambukizi ya malaria ni wastani wa mtu mmoja kwa kila mia moja ikilinganishwa na wastani wa watu arobaini kwa kila mia moja kwa mwaka 2005. Kwa kuwa malaria ilikuwa ni miongoni mwa maradhi yanayoongoza kwa vifo, kupungua kwa maradhi haya kutachangia sana katika kuimarisha wastani wa umri wa kuishi kwa wananchi wa Zanzibar. Nawashukuru wananchi kwa ushirikiano wao na wafanyakazi wa Wizara ya Afya katika zoezi la upigaji dawa za mbu majumbani mwao, ambao umefanikisha mpango wa kupunguza malaria.

Hapa sauti ya mtoto ilisikika.

Nadhani anafurahia huyo, maana si jambo dogo hilo. Malaria ilikuwa inamuudhi kila mtu. Kwa sasa nchi yetu imekuwa ni chuo ambapo wataalamu kutoka nchi mbali mbali duniani wanakuja kujifunza mikakati ya kudhibiti malaria.

Mhe. Spika, moja ya maradhi thakili yanayoathiri sehemu kubwa ya watu, wetu hapa, Kusini mwa Jangwa la Afrika pia ni UKIMWI. Maradhi haya yameendelea kuathiri kwa kiasi kikubwa rika la nguvu kazi na hivyo kurejesha nyuma juhudi za ukuzaji wa uchumi na kuongeza gharama za huduma za kijamii. UKIMWI pia umekuwa chanzo kikubwa cha kuporomoka kwa wastani wa umri wa kuishi kwa nchi nyingi katika eneo hilo. Zanzibar kwa upande wake, imeendelea kupata mafanikio katika mapambano dhidi ya maradhi hayo. Kiwango cha jumla cha maambukizi kimebakia kuwa chini ya asilimia moja. Utafiti wa mwaka 2008 unaonesha kuwa kiwango hicho cha jumla ni asilimia 0.6. Hata hivyo, maambukizi bado yamebaki kuwa ya juu kwa makundi maalum kama vile watumiaji wa madawa ya kulevya na watu wanaojihusisha na ngono za jinsia moja.

Tatizo jengine muhimu na la hatari ni kupoteza maisha watoto wachanga na kinamama wanapojifungua pamoja na watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Sote tuna jukumu la kuhakikisha kuwa baada ya uchungu wa uzazi, watoto hawapotezi uhai kwa maradhi yanayoweza kutibika. Kwa wenzetu nchi zilizoendelea, ni nadra sana mtoto mchanga kufariki. Katika kipindi cha miaka mitano ya uhai wa Baraza hili, vifo vya watoto wa chini ya umri wa miaka mitano vimepungua kutoka wastani wa vifo 101 hadi vifo 79 kwa kila watoto 1000. Hali hii bado si ya kuridhisha.

Sambamba na upunguzaji wa vifo vya watoto wadogo, serikali pia imefanikiwa kupunguza vifo vya mama waja wazito kutoka 377 hadi vifo 280 kwa kila waja wazito 100,000. Kwa jumla, mafanikio yote haya yamesaidia kuongeza wastani wa umri wa kuishi, ingawa juhudi kubwa zaidi zinahitaji kuendelezwa.

Elimu:

Mhe. Spika, baada ya afya njema, jambo jengine muhimu kwa maendeleo ya mwanadamu ni elimu. Ni kupitia jamii yenye siha nzuri na iliyoelimika vyema ndio maendeleo hufikiwa kwa haraka.

Kwa kutambua umuhimu wa elimu, Serikali ya Awamu ya Sita iliweka mkazo maalum katika kuwapatia watoto wa Zanzibar fursa ya elimu na kuinua ubora wa elimu hiyo. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia mafanikio makubwa katika juhudi zetu hizi. Leo hii kila mtoto wa Zanzibar mwenye umri wa kwenda skuli anayo fursa ya kujiandikisha na kusoma. Bado kila mtoto anapata elimu ya lazima bila ya malipo, kutoka darasa la kwanza hadi kidato cha pili (darasa la kumi). Mipango ilio mbele yetu ni utekelezaji wa lengo la elimu ya lazima kuwa hadi kidato cha nne. Tunaishukuru sekta binafsi katika utoaji wa elimu ingawa skuli nyingi za binafsi zimeelekezwa katika elimu ya maandalizi na msingi. Mashirikiano na sekta binafsi ni makubwa, pia katika elimu ya juu ambapo viwili kati ya vyuo vikuu vitatu vilivyopo Zanzibar ni vyuo binafsi.

Miongoni mwa mafanikio yaliopatikana ni kuongezeka kwa mtandao wa skuli za maandalizi, skuli za msingi na sekondari baina ya mwaka 2005 na 2009 kama ifuatavyo:

Maandalizi	205 - 232
Msingi	140 - 167

Sekondari 50 – 95 na bado ujenzi unaendelea.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri wananchi nao wameitikia vyema wito wa kuwapeleka watoto skuli. Idadi ya watoto katika skuli za msingi imeongezeka kutoka 208,000 mwaka 2005 hadi 220,000 mwaka 2009. Jambo la kufurahisha zaidi ni kwamba idadi ya watoto wanaume na wanawake karibuni inalingana. Kwa upande wa skuli za sekondari, idadi ya wanafunzi katika kipindi cha 2005-2010 imeongezeka kutoka 64,980 hadi 77,958. Idadi ya wanafunzi wanawake imezidi ile ya wanaume kwa asilimia 10.4. Hali ya kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi, pia imejitokeza kwa ngazi ya sekondari ya juu (*Form V na VI*) ambapo idadi ya wanafunzi imeongezeka kwa asilimia 72 kutoka 2,818 mwaka 2005 hadi wanafunzi 4,844 mwaka 2009. Katika ngazi hii hata hivyo, idadi ya wanafunzi wa kiume ni kubwa kwa asilimia 14.2 zaidi ya ile ya wanafunzi wa kike. Kwa upande wa elimu ya juu idadi ya wanachuo katika vyuo vikuu vitatu ni 3,624 ambapo wanaume ni 2,076 na wanawake 1,548.

Sasa inaonesha kwamba kila wakiendelea watoto wetu ukusoma wanawake wanapungua kwa uiyano. Kwa mtizamo wa haraka haraka nafikiri wengi wanachumbiwa. Hilo ni jambo ambalo linafaa tulitizame vizuri zaidi. Kwa sababu pia tunaweza kuwachumbia wakati wanaendelea kusoma.

Ili kuhakikisha ubora wa elimu, serikali imeongeza idadi ya walimu kutoka 8,790 mwaka 2005 hadi 9,798 mwaka 2009. Pia, imempatia kila mwanafunzi dawati na vitabu vya rejea kwa masomo yote ya sayansi na hesabati kwa sekondari. Tunaamini kwamba ubora wa elimu ya sekondari utaimarika zaidi baada ya kukamilika mradi wa zile skuli 19 mpya unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Mhe. Spika, katika kipindi hicho cha miaka mitano, serikali imeanzisha vituo vya elimu mbadala kwa wanafunzi ambao hawakubahatika kumaliza ule mkondo wa kawaida. Kwa upande mwengine, mkazo mkubwa uliwekwa katika elimu ya ufundi, sayansi na elimu ya vyuo vikuu. Serikali imeanzisha vyuo viwili vipya na vya kisasa vya mafunzo ya amali, kimoja Pemba na chengine Unguja.

Mhe. Spika, kama nilivyosema awali, elimu ni chachu kubwa ya kujenga jamii ya kisasa yenye kuishi kwa matumaini na iliyoondokana na unyonge na umaskini. Uwekezaji wote huu uliofanywa na serikali katika kipindi cha Awamu ya Sita umelenga katika yote hayo. Sasa ni matumaini yangu, kuwa uwekezaji wetu huu katika rasilimali watu utasaidia sana hapo baadae katika kuharakisha maendeleo ya Wazanzibari wote.

Maji Safi na Salama:

Upatikanaji wa maji safi na salama ni muhimu kwa afya za wananchi. Hadi mwaka 2009 asilimia 86 ya Wazanzibari wote waliweza kupata huduma ya maji safi na salama. Upatikanaji huo umefikia asilimia 95.9 kwa maeneo ya mijini na asilimia 80.7 kwa maeneo ya vijijini. Tunataraji kukamilika kwa mradi mkubwa wa maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi mwezi Agosti/Septemba mwaka huu unaotekelezwa kwa ushirikiano na Serikali ya Japan kutalimaliza tatizo hilo mkoani humo kwa kiasi kikubwa.

Maendeleo ya Nyumba:

Katika kustawisha maisha ya wananchi wetu, niliahidi nilipochukua madaraka mwaka 2000 kuwa tutakamilisha majenzi ya nyumba za maendeleo za Michenzani zilizoanzwa na Rais wetu wa Kwanza, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Kwa bahati nzuri kazi hiyo imemalizika na kilio cha wananchi wote waliovunjiwa nyumba zao zaidi ya miaka 38 iliyopita nacho kimeisha, baada ya kukabidhiwa nyumba mpya mwanzoni mwa mwaka huu. Kwa hili mimi mwenzenu nimepata faraja kubwa sana. Lazima nikiri kwamba, aliyeamrisha kuvunja nyumba zile alikuwa bwamkubwa wangu, lakini kwa nia njema ya kuwajengea nyumba zilizo bora zaidi, lakini kwa bahati mbaya hakuwahi kuzimaliza nyumba zile Mwenyezi Mungu amemuhitaji.

Sasa hili lilikuwa ni deni, na miaka yote lilikuwa linanikereketa sana, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu kanipa nafasi na ninawashukuru na nyinyi wenzangu nyote pamoja na wananchi wote wa Zanzibar tumeweza kukamilisha hili alililoliacha bwamkubwa wetu. Mwenyezi Mungu amlaze mahala

pema peponi. Kwa kweli eneo hilo la Michenzani sasa lina mandhari ya kupendeza na hivi juzi tumeanza mradi wa barabara, tunapambia pambia ili mambo yawe mazuri zaidi.

Wakati huo huo, ujenzi wa nyumba za maendeleo kule Mpapa unaendelea vyema na tegemeo letu ni kwamba, baada ya muda mfupi nao pia utakamilika.

Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Sita, pamoja na kuendeleza nyumba za maendeleo za makazi ya watu, imefanikiwa pia kujenga majengo mbali mbali ya kisasa ya wizara na mashirika ya umma. Aidha, tumefanya marekebisho makubwa kwa majengo mbali mbali kama hospitali na skuli. Majengo mapya ni Jengo la Vitega Uchumi la *ZSTC*, Majengo ya *ZSSF* Unguja na Pemba, Makao Makuu ya Wizara ya Fedha na Uchumi Unguja, Nyumba ya Wageni Pemba, Makao Mkuu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Unguja, Vituo vya Amali Unguja na Pemba, Jengo jipya la Chuo cha Uongozi wa Fedha Chwaka, Jengo la Makao Makuu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Jengo la Benki ya Damu – Sebleni, Jengo la Maabara ya Afya na Jamii Pemba, Jengo la Mradi wa Malaria Mombasa na Mwanakwerekwe, Hospitali ya KMKM Kibweni.

Vile vile Kituo cha *VCT* Pemba kinaendelea, Chuo cha Afya Mbweni, jirani hapa, Jengo la Elimu ya Afya, Nyumba za Madaktari, Radio Jamii Micheweni, Kituo cha Huduma za Upimaji Ukimwi na Ushauri Nasaha Hospitali ya Mnazi Mmoja Unguja, Jengo la Uhandisi la Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Mombasa, Unguja, Nyumba ya Serikali Micheweni, Afisi ya *DPP* Unguja, Makao Makuu ya *ZIPA* Maruhubi Unguja. Kubwa zaidi kwa sababu hili limetia fora, Jengo jipya la fahari la Baraza la Wawakilishi Mbweni, Jengo la Afisi ya Mufti Mazizini Unguja na Kituo cha Mafunzo ya Kilimo na Maabara Kizimbani.

Mengine ni Majengo ya *MACEMP* Unguja na Pemba, Majengo ya Afisi ya miradi ya huduma za Kilimo Maruhubi na Machomane Pemba, na hapo Mazizini mkabala na Makao Makuu ya Elimu kuna jengo kubwa pale la *ZRB* (ujenzi unakaribia kumalizika). Majengo mengine mengi tumeyashughulikia, lakini sasa, liko moja hapa lazima nilitamke. Majengo mapya ya Chuo Kikuu cha Zanzibar, (*SUZA*). (*Makofi*)

Majengo yaliyofanyiwa ukarabati mkubwa ni Afisi ya Rais Ikulu, Kibweni *Palace* na Ikulu Ndogo Wete na Chake Chake. Hapa kwa niaba yenu nataka nimpongeze sana Mama Shadya. Kwa sababu alisimama kidete kuhakikisha kwamba, lile jengo la Ikulu na majengo haya yanaimarishwa pengine au vyenginevyo baadhi yao mngekwishadondoka hivi sasa. hivi karibuni kuna mtu alikuja pale akaniuliza, aa, hii kazi kubwa inayofanywa ya kutengeneza hili jengo kwa nini mnapoteza muda? Nikamuuliza kwa nini? Akasema nyinyi mnamaliza muda si kumuachia huyo atakaekuja? Nikamuangalia usoni nikampima fikra yake nikaona sasa huyu ana mawazo yale yale ya kizamani. Mawazo ya kileo unajenga unaimarisha halafu unawajengea wanaokuja pia. Kwa sababu wazee wetu wasingepanda midoriani ambayo hawajaila, sisi tusingekula madoriani.

Lakini pamoja na yote hayo, katika kuendeleza mandhari ya mji wa Unguja, Mji Mkongwe, kwa kushirikiana na Aga Khan Trust, tumeifanyia matengenezo makubwa bustani ya Forodhani na sasa hivi tumeigeuza kuwa ni kivutio cha fakhari kwa wageni na wenyeji pia.

Utawala Bora:

Mhe. Spika, sasa nataka kidogo nizungumzie Utawala Bora. Tokea nimeingia madarakani mwaka 2000 nimeweka mkazo maalum kuhakikisha kuwa kunakuwa na utawala bora nchini ikiwa ni msingi wa kudumisha uhuru wetu na kuendeleza demokrasi. Ninafuraha kuwa, kuanzia mwaka 2001 nchi yetu imepiga hatua kubwa katika uimarishaji wa misingi ya utawala bora. Kati ya mwaka 2000 na 2005 hatua zifuatazo zimechukuliwa katika mwelekeo huo.

Tumeanzisha wizara maalum ya mambo ya Katiba na Utawala Bora ambayo imesimamia uundaji wa Tume Huru ya Uchaguzi inayojumuisha wajumbe kutoka vyama vikuu vya siasa nchini. Kadhalika tumeanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambalo tulilitumia katika uchaguzi mkuu wa 2005

kwa mafanikio makubwa. Kwa mara ya kwanza katika historia ya Zanzibar tumeanzisha mfumo wa kuwa na Vitambulisho vya kisasa vya Wakaazi wa Zanzibar. Aidha, kila mpiga kura halali aliomo ndani katika daftari la kudumu amepatiwa kitambulisho cha kisasa cha kupigia kura tu peke yake, ambacho kimeanza kutumika kwa mafanikio makubwa mwezi uliopita katika kura ya maoni.

Katika kuhakikisha upatikanaji wa haki za raia, tumerekebisha mfumo wa Mahakama na kuufanya uwe bora zaidi kwa kurekebisha baadhi ya sheria na kanuni na kuzipatia Mahakama uhuru zaidi wa kuendesha kazi zake, kuongeza idadi ya Mahakimu pamoja na kuyakarabati majengo yao.

Serikali ya Awamu ya Sita, pia, imeanzisha Afisi maalum ya Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Mashtaka (*DPP*). Tumeweza vile vile kufanya marekebisho ya sheria mbali mbali za jinai. Tume ya Haki za binaadamu imefunguliwa hapa Zanzibar kushughulikia ukiukwaji wa haki za binaadamu.

Mhe. Spika, nilipoingia madarakani, nilianzisha Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ili kusimamia na kulinda haki zao pamoja na kushajiisha jamii kuziheshimu na kuzitekeleza haki hizo. Wizara imekuwa ikiendelea kutoa elimu na mafunzo kupitia vyombo vya habari na kuwasikiliza wanawake na watoto wenye matatizo na kuyapatia ufumbuzi kwa kutoa ushauri nasaha kwa kushirikiana na taasisi nyengine kwa nia ya kuleta utulivu, amani na maendeleo katika familia.

Serikali ya Awamu ya Sita, kwa kupitia wizara hiyo, inaendelea kuwajengea uwezo wanawake kwa kuwapa fursa ya kuanzisha na kuendeleza biashara kwa lengo la kuinua kipato chao na kuinua uchumi, kwani wakiwezeshwa wanawake wanaweza. Mashirika ya *UNICEF* na *ILO* yametoa mashirikiano makubwa katika kuhakikisha watoto wa Zanzibar wanapata haki zao za msingi kwa kuweka sheria za kazi na kupiga vita ajira za watoto na kuwawezesha wanawake kujiunga katika vikundi ili waweze kujikimu kimaisha kwa kufanya kazi na biashara. Natoa shukurani nyingi kwao na watendaji wao waliopo Zanzibar na Tanzania Bara. Pia, tumekuwa tukiwajali watu wenye ulemavu kwa kushirikiana na kusaidiana na taasisi zao mbali mbali ili waweze kujimudu na kujiendesha kimaisha. Aidha, tunatoa mashirikiano makubwa kwa wafanyakazi waliostaafu na kujiunga pamoja.

Ushirikishwaji na Uwezeshaji wa Wananchi:

Mhe. Spika, misingi ya kidemokrasia inayofuatwa na nchi yetu inahitaji wananchi wenyewe kushiriki katika kupanga na kutekeleza mipango yao ya maendeleo. Ushiriki huo hufanyika kupitia vikundi mbali mbali, utoaji wa maoni kwenye vikao na warsha, lakini pia kupitia Wawakilishi wao hapa Barazani na katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa upande wa Baraza hili, juhudi za kuliimarisha zimeendelezwa kwa kupatiwa watendaji wenye ujuzi na vifaa vya kisasa vya kazi. Aidha, mafunzo mbali mbali kwa njia za semina na ziara za ndani na nje ya nchi zimetolewa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza. Mashikirikiano na Mabunge mengine ulimwenguni yameimarishwa ili kuwajengea uzoefu Wajumbe na Wafanyakazi wa Baraza.

Ili kulipa haiba na hadhi inayostahiki Baraza la Wawakilishi, *Alhamdulillah* tumekamilisha ujenzi wa jengo hili jipya la Baraza ambalo leo tunalitumia likiwa ni mali ya wananchi wote wa Zanzibar.

Baraza la saba la Wawakilishi linamaliza muda wake kwa mafanikio makubwa. Baraza hili limepitisha jumla ya miswada ya sheria 56 na sera 12 na kujibu maswali 1,640 yaliyoulizwa. Baraza hili litakumbukwa kihistoria kuwa ni Baraza lililoweka misingi ya kudumu ya umoja, mshikamano, utulivu na amani ya Zanzibar. Limefanya maamuzi mazito kwa uadilifu na kujijengea heshima kubwa. Baraza hili pia limesimamia vyema madhumuni na malengo ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964 kulinda uhuru wa Zanzibar na watu wake, kulinda utu, umoja na heshima ya Wazanzibari wote ya kujiamulia mambo yao yanayohusu nchi yao na uchumi wao. (*Makofi)*

Mhe. Spika, katika kuwawezesha wananchi kiuchumi, mtakumbuka kuwa Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na mimi tulianzisha mfuko maalum, maarufu kama Mfuko wa JK na AK. Hadi mwezi Juni mwaka huu jumla ya wananchi 658 wamenufaika kwa kukopeshwa jumla ya shilingi 1,345.90 milioni kutoka Mfuko huu. Lengo la mikopo kutoka mfuko

huu na ile Mifuko ya *PRIDE*, *WEDF*, *SELF* na Mfuko wa Kujitegemea ni kuwapatia mikopo nafuu wananchi wazalishaji wadogo wadogo ili kuendeleza miradi yao mbali mbali. Uanzishaji huu wa mifuko mbali mbali unahitaji kusaidiwa na uongezaji wa elimu na utaalam kwa wajasiriamali hao ili mikopo hiyo iwe endelevu na yenye tija zaidi katika kuwaongezea wananchi wetu kipato.

Mhe. Spika, katika kuimarisha mawasiliano na ushiriki wa makundi mbalimbali katika kuleta maendeleo ya nchi, serikali imeanzisha Baraza la Biashara la Zanzibar (*ZBC*) lenye wajumbe sawa kutoka serikalini na sekta binafsi kwa lengo la kusikiliza maoni ya kuimarisha mazingira ya kibiashara na kiuchumi nchini. Kwa nafasi yangu ya Urais wa Zanzibar mimi ndie mwenyekiti wa *ZBC*. Hii ni ishara ya umuhimu unaowekwa na serikali juu ya mashirikiano hayo na sekta binafsi. Hadi sasa, *Zanzibar Bussines Council* imeshafanya kwa mafanikio makubwa vikao vinne. Mashirikiano pia yameimarika baina ya serikali na taasisi zisizo za kiserikali.

Kuimarika kwa Ushirikiano wa Kimataifa:

Mhe. Spika, nchi yetu, kupitia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa, Umoja wa nchi Huru za Afrika, Jumuiya ya nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya mbali mbali za Kikanda. Mahusiano mazuri na nchi za nje ni jambo jema na lenye manufaa ya kiuchumi, kijamii na usalama. Kwa bahati mbaya, serikali ya awamu ya sita iliingia madarakani mwaka 2000 hali ya kuwa Zanzibar imesusiwa na wengi kati ya Washirika wetu wa Maendeleo kwa sababu za kisiasa. Kipindi cha miaka kumi ya 2000 hadi 2010, kimeshuhudia kuimarika sana kwa uhusiano wetu na nchi hizo pamoja na mashirika ya kimataifa. Kuimarika kwa mahusiano hayo ni kielelezo cha kukubalika kwa serikali yetu, uongozi wake na kuheshimiwa demokrasia nchini.

Hali ya Kisiasa:

Mhe. Spika, kwa miongo mingi nchi yetu ilikuwa haijashuhudia utulivu endelevu wa kisiasa. Tunahitaji utulivu wa kudumu wa kisiasa ili tuweze kuwa na maendeleo endelevu. Hakuna muwekezaji yeyote makini atakaewekeza fedha nyingi katika nchi ambayo utulivu wake ni wa kimiongo, unaingia mashakani kila baada ya miaka mitano wakati wa uchaguzi.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia fursa ya kupata utulivu wa kudumu nchini kwetu kupitia mazungumzo baina yangu na Maalim Seif Sharriff Hamad, Katibu Mkuu wa *CUF* hapo tarehe 5 Novemba mwaka jana, Ikulu, Zanzibar. Tulifanikiwa kufikia maridhiano ya kumaliza uhasama wa kisiasa Zanzibar na kusameheana. Najuwa tumeshapongezwa sana, kuhusiana na maridhiano hayo. Hata hivyo, naomba nichukue fursa hii tena kumpongeza sana Maalim Seif na chama chake kwa kufanya maamuzi hayo ya kijasiri ya kuitambua serikali yangu, lakini pia kuwa tayari kuleta maridhiano, na pia kukubali kuwa wananchi wenyewe ndio wawe waamuzi wa mwisho juu ya mustakabali wa nchi yetu.

Mhe. Spika, inaonekana kuwa moja ya tatizo linalochangia hali ya kutofahamiana ni mwamko mkubwa wa kisiasa kwa wananchi wetu unaoongezwa nguvu na kukaribiana kwa kiasi fulani kwa matokeo katika chaguzi mbali mbali. Tulihitaji kufikira njia mpya bora zaidi, na itakayokubalika na wananchi walio wengi ili kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hilo. Najua kuwa miongoni mwetu zilikuwapo fikra na rai tofauti juu ya namna ya kukabiliana na hali hio. Wapo wachache wanaoamini kuwa hali hiyo ingejirekebisha yenyewe na hivyo utaratibu wa sasa wa chama kinachoshinda kuunda serikali peke yake uendelee japo kuwa umetuletea matatizo mengi na kwa muda mrefu.
Wapo, pia, walioamini kuwa palihitajika njia mbadala ya kuongoza nchi yetu. Kati ya hawa nami nikiwemo, tuliona kuwa njia hiyo mbadala ni kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoundwa na vyama vyote vilivyopata ridhaa ya wananchi kuwawakilisha katika Baraza la Wawakilishi. Aidha, serikali hiyo iongozwe na chama kilichopata kura nyingi zaidi za urais katika Uchaguzi Mkuu. Maamuzi kama haya sio madogo kwa mustakabali wa nchi. Vyama vyetu vikuu viwili, CCM na *CUF*

vilikubaliana juu ya haja ya maamuzi hayo kufanywa na wananchi wenyewe tena kwa utaratibu unaotumika kimataifa. Moja wapo ya njia za kufanya maamuzi kama haya ni kupitia kura ya maoni (*Referendum*) ambapo wananchi huamua kati ya fursa zilizopo. Nasi hapa Zanzibar tukakubaliana kutumia njia hiyo kupata maamuzi ya wananchi wenyewe.

Mhe. Spika, tarehe 31 Julai mwaka huu, wiki mbili zilizopita, wananchi wa Zanzibar walishiriki kupiga kura ya maoni na kuchagua wanachokitaka. Matokeo ya kura hiyo yalikua wazi kwa thuluthi mbili ya waliopiga kura kuamua kuwa serikali ijayo iwe ya umoja wa kitaifa. Idadi hii inamaanisha kuwa kati ya kila Wazanzibari watatu waliopiga kura, wawili wamekubali kuanzishwa kwa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu. Hata hivyo, wapo wananchi wachache waliotaka utaratibu wa sasa uendelee.

Kwa kutilia maanani namna ambavyo wananchi walielimishwa kwa muda mfupi juu ya kura ya maoni na kushiriki kwa wingi na utulivu mkubwa katika upigaji wa kura hiyo. Natoa pongezi za dhati kwa Kamati ya Watu Sita ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Utekelezaji wa Azimio la Baraza kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar iliyoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Ali Mzee Ali kwa juhudi zao katika kufanikisha zoezi hilo. (*Makofi)*

Lakini zaidi pamoja na kwamba Baraza tunalivunja leo, kamati hii itahitajika kuendelea na shughuli fulani fulani ambazo zitaweka vizuri utaratibu huo ambao tutakwendanao mbele ya safari. Lakini pia kwa kuzingatia hekima za wazee wetu inayosema wengi wape, katika ile kura ya maoni sasa, sote kwa pamoja tunapaswa kuyaheshimu maamuzi ya wengi.

Naomba niwashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa kutoa maoni yao kwa njia ya utulivu, kistaarabu na ukomavu mkubwa wa kidemokrasia. Nawashukuru zaidi walio wengi ambao wamekubaliana na mageuzi ya namna ya kuongoza nchi yetu. Sote kwa pamoja tumeandika historia mpya nchini petu. Natumai itakuwa historia nzuri itakayomnufaisha kila mmoja wetu, tuliopo sasa na vizazi vijavyo. Kwa vyama vyetu vya siasa maamuzi haya ya wananchi ni maelekezo yao kwetu. Ni ushindi wa wananchi wote sio wa wanasiasa wala sio wa vyama vya siasa.

Aidha, hatupaswi kuyabeza maoni ya wachache waliotaka kuendelea na utaratibu wa sasa. Tujue tu kuwa kwenye mabadiliko sio wote kuyakubali kwa haraka. Wengine mpaka waone wenyewe faida zake. Kwa hivyo basi, hali hiyo iwe ni changamoto kwetu sote tulio wengi kuhakikisha kuwa historia isiyopendeza nchini kwetu haijirejei ili tuwape moyo hao wenzetu wenye hofu, ili waungane nasi katika safari hii yenye matumaini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya mchakato wa kura za maoni na walio wengi kuunga mkono muundo mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, narejea tena muundo mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)* Maana kuna wengine walikuwa wanafikiria kwamba Serikali ya Mapinduzi sasa ndio basi. Kasema nani? Hili bora nilirejee tena. Baada ya mchakato wa kura ya maoni na walio wengi kuunga mkono muundo mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, juzi tarehe 9 Agosti siku tatu zilizopita, Baraza lako tukufu kwa kauli moja lilipitisha Mswada wa Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar. Marekebisho haya ya kihistoria yataruhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa iundwe mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu. *(Makofi)*

Sasa nataka nichukue fursa hii kwanza kukupongeza wewe binafsi Mhe. Spika, pamoja na Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Nawapongeza sana kwa uamuzi wenu wa kizalendo. Kama tulivyotangulia kusema bila ya shaka yoyote uamuzi wenu huo utaingia katika vitabu vya historia ya Zanzibar itakayokumbukwa kwa miaka mingi ijayo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nchi yetu inakabiliwa tena na Uchaguzi Mkuu tarehe 31 Oktoba mwaka huu. Kwa upande wetu serikalini tunaendelea vyema na matayarisho ya uchaguzi huo kwa kukiwezesha chombo chenye dhamana yake Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Matumaini yangu kuwa tume, vyama vya siasa na wananchi wote tutaungana kuhakikisha kuwa uchaguzi wa mwaka huu unaandika historia mpya nchini kwetu, historia inayoendana na maridhiano yaliyopo ya kisiasa. *(Makofi)*

Nia yetu ni kuwa na historia ya uchaguzi wa kuaminiana, uchaguzi wa kistaarabu na uchaguzi ulio safi na huru kwenye macho yetu sote wapiga kura na waangalizi watakaokuwepo. Uchaguzi huu utabeba matumaini makubwa zaidi ya wananchi kimaendeleo, kiutulivu na kiuchumi. Naomba sote tuhuishe matumaini yao kwa salama na amani. *(Makofi)*

Mwisho Mhe. Spika, miaka 10 katika historia ya nchi ni kipindi kifupi sana. Kwa mujibu wa katiba yetu, Rais ndie kiongozi wetu wa nchi, lakini miaka kumi ya uongozi wa nafasi ya juu katika nchi ni muda mrefu sana wa dhamana iliyo nzito. Dhamana hiyo inampa dhima rais kutumia mamlaka aliyopewa kuhakikisha, (i) Usalama na amani ya nchi inadumishwa, (ii) Demokrasia na haki za wananchi wote zinalindwa, (iii) Nchi inapata maendeleo na kuinua ustawi wa jamii kwa jumla, (iv) Kudumisha umoja na maslahi ya Zanzibar ndani ya Muungano pamoja na kujenga mahusiano bora na majirani, na nchi na mashirika ya nje. Zaidi ya yote hayo, Rais ana dhamana ya kuitetea, kuilinda na kuitekeleza Katiba ya nchi. Sasa hizo zote ni dhamana nzito. *(Makofi)*

Tarehe 8 Novemba, 2000 mara baada ya kuapishwa na kukabidhiwa dhamana ya kuiongoza nchi yetu, nilitoa hotuba fupi pale Uwanja wa Amaan na kwa leo napenda nijinukuu mwenyewe. Katika sehemu ya hotuba hiyo nilisema hivi:

"Ndugu wananchi, leo nathubutu kusimama mbele yenu kwa sababu wananchi wa Zanzibar wametumia haki yao ya kikatiba ya kumchagua Rais wanayemtaka. Wakati napokea imani yenu kwa heshima na unyenyekevu kuwa Rais wa Zanzibar, sina budi kupokea wito wa wananchi wa kutaka mabadiliko. *Change* ndio mabadiliko, tulitangulia sisi hapa. *(Makofi)*

Nilipokuwa nafanya kampeni ya kuomba kura zenu kwa niaba yangu na niaba ya chama changu, niliendelea kusisitiza juu ya umoja, amani na utulivu ndani ya nchi yetu. Leo nasimama tena mbele yenu kwa sababu mmekubali wito huo na kunichagua mimi kuwa Rais wenu. Sasa baada ya kunichagua mimi kwa kura nyingi sana na kunipa ushindi mkubwa ni dhahiri kwamba nyote kwa pamoja mmechagua umoja, amani na utulivu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa kuniamini kwa kazi kubwa ya utekelezaji wa chaguo lenu la umoja, amani na utulivu. Napenda niwaombe wananchi wote ushirikiano wenu." *(Makofi)*

Mhe. Spika, maneno haya niliyasema tarehe 8 Novemba, 2000 Uwanja wa Amaan. Wengi wenu mlikuwepo siku ile au wengine mmeona katika televisheni, au mmesikia katika vyombo vya habari.

Sasa baada ya maelezo hayo sina budi sasa kuwashukuru sana wananchi wote wa Zanzibar kwa kunikubalia ombi langu la kuchagua umoja, amani na utulivu na kuniunga mkono katika kipindi chote. *(Makofi)*

Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita naamini kwamba nimetumia uwezo wangu kuyatekeleza yote haya kwa kadri Mwenyezi Mungu Rahim alivyonijaalia. Lakini sikufanya kazi hiyo kubwa peke yangu ila nimeshirikiana na wananchi wote wa Zanzibar, viongozi wenzangu wa chama changu serikalini na nje ya serikali. Nimeshirikiana na kufanya kazi kwa karibu sana na Marais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Mstaafu Benjamin William Mkapa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Nawashukuru wote kwa dhati kwa mashirikiano, msaada wao na ushauri wao kwangu kwa muda wote. *(Makofi)*

Namshukuru mzee wetu Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Ali Hassan Mwinyi. Namshukuru pia Rais Mstaafu wa Zanzibar, Mzee Aboud Jumbe Mwinyi kwa kuanzisha Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Wakati huo huo, namshukuru Rais Mstaafu wa Zanzibar, Mhe. Dk. Salmin Amour Juma. *(Makofi)*

Nimebahatika pia kufanya kazi kwa karibu sana na Marehemu Dk. Omar Ali Juma wakati akiwa Makamo wa Rais chini ya Mhe. Benjamin William Mkapa. Mwenyezi Mungu kamhitaji na ni wajibu wetu. Namuombea maghufira na malazi mema. Amin.

Nawashukuru pia Mhe. Dk. Ali Moh'd Shein, Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru viongozi wengine wote wa kitaifa walio madarakani na wastaafu niliowahi kufanyakazi nao, mawaziri na watendaji wengine. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa mujibu wa utaratibu wa uongozi wa nchi yetu, nchi inaongozwa na mihimili mitatu, ule wa Utawala *(Executive)* unaoongozwa na Rais, wa Kutunga Sheria *(Legislature)* ndio hii nyinyi hapa Baraza hili tukufu unaoongozwa na Spika. Pia mhimili wa Kusimamia Haki *(Judiciary)* unaoongozwa na Mhe. Jaji Mkuu.

Sasa kwa mujibu wa katiba yetu kama nilivyosema awali kiongozi wa nchi ni Rais. Naomba sasa nitumie fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Pandu Ameir Kificho, Spika wa Baraza hili linalomaliza muda wake na Mhe. Hamid Mahmoud Hamid, Jaji Mkuu wa Zanzibar. Nasema kutoka ndani ya moyo wangu kuwa katika kipindi chote cha uongozi wangu wa nchi nimepata bahati ya kufanya kazi kwa mashirikiano makubwa kutoka kwenu. *(Makofi)*

Nimebahatika kupata maoni na ushauri wenu muhimu ulionisaidia sana katika kufanya maamuzi mengine yakiwa magumu. Wakati wote ukaribu wenu umekuwa ni ngao muhimu kwangu hata kwa kujua tu kwamba wenzangu nyinyi mnaniunga mkono na mko pamoja nami. Nakushukuruni sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda pia kumshukuru Waziri Kiongozi, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Naibu Waziri Kiongozi, Mhe. Ali Juma Shamuhuna, pamoja na Mawaziri wote waliofanya kazi chini yangu. Nataka nikiri kwamba mawaziri wote tuliofanya kazi pamoja kwa mashirikiano, kwa utiifu na ushauri wenu kwangu uliowezesha kuvusha nchi yetu katika muda wote huo. *(Makofi)*
Nawashukuru sana Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Makamishna, Wakurugenzi na viongozi na wafanyakazi wote wa serikali kwa utendaji wao mzuri uliotufikisha hapa tulipo kwenye mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Natoa shukurani pekee kwa maofisa na wafanyakazi katika Afisi ya Rais Ikulu. Nawashukuru kwa uaminifu wao kwangu, ushirikiano na kazi nzuri wakati wote na uvumilivu wao katika kazi. Nawaambia ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, shukurani zangu nyingi pia ni kwa wakuu wa vikosi na askari wote wa vikosi vyetu vya ulinzi na usalama kwa utiifu wao kwangu kama kiongozi wao na kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuwafanyia wananchi wenzao wa Zanzibar katika kudumisha ulinzi na usalama wetu pamoja na nchi yetu. Nasema ahsanteni. *(Makofi)*

Shukurani zangu maalum zinakwenda kwa wananchi wote kwa kuniamini, kunipa fursa ya kuwatumikia na kunistahamilia wakati nchi yetu ilipopita vipindi vigumu. Natumai neno la ahsante litabeba uzito wa kutosha wa shukurani zangu kwao. *(Makofi)*

Nakishukuru pia Chama changu cha Mapinduzi kwa kuniamini na kunipa fursa hii adhimu. Aidha, nawashukuru viongozi wa dini na taasisi zisizokuwa za kiserikali kwa kushirikiana nami katika kipindi changu chote kuhubiri amani, umoja na utulivu nchini mwetu. *(Makofi)*

Pia nawashukuru mabalozi wa nchi za nje waliofanya kazi Zanzibar katika kipindi cha awamu ya sita na pia waliokuwepo Tanzania Bara kwa kushirikiana na sisi kwa urafiki na kufahamiana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa niruhusu pia nitoe shukurani nyengine maalum kwa familia yangu. Familia yangu imekuwa ndio mhimili wangu na chachu ya mafanikio yangu. Namshukuru sana mama yangu mzazi Mama Fatma Karume, namshukuru kwa namna ya kipekee mke wangu Mama Shadya Karume,

nawashukuru sana wanangu, wajukuu na wanafamilia wote kwa kuniunga mkono bila ya ukomo wala kuchoka katika kipindi chote cha mimi kuiongoza nchi yetu. Familia yangu imenistahamilia na imevumilia mengi wakati nikitumia muda wangu mwingi kuwatumikia wananchi wenzangu. *(Makofi)*

Sasa nataka nikiri kwamba maisha yao katika kipindi hicho hayakuwa mepesi hata kidogo, kwa vile waliokasirika nami wakati huo joto lao lote liliishia kwa familia yangu kama ilivyo kawaida kwa wanasiasa wengine. Lakini pamoja na yote hayo, walikuwa nami katika kuitumikia nchi yetu na chama chetu kwa uwezo wao wote. Nasema ahsante. *(Makofi)*

Namshukuru sana ndugu yangu mzazi Balozi Ali Abeid Karume, pamoja na ndugu zangu wazazi wa kike, jaama zangu na marafiki zangu wote kwa msaada wao kwangu. Nawashukuru tena wananchi wote wa Zanzibar na Watanzania wote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, muda wangu wa kuitumikia nchi yetu kama rais unafikia ukomo wake mara baada ya Uchaguzi Mkuu wa tarehe 31 Oktoba mwaka huu, baada ya hapo tutapata kiongozi mwengine.

Nimeeleza mafanikio makubwa tuliyoyapata miaka kumi inayomalizika. Hata hivyo, bado nchi yetu inakabiliwa na changamoto kadhaa. Katika kukabiliana na changamoto hizo serikali yetu imeweza kuweka misingi madhubuti ya maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Misingi hii inahitaji kutunzwa, kuuimarishwa na kuendelezwa kwa kasi zaidi.

Kwa kuwa uchumi wetu unahitaji kasi zaidi ya mageuzi kuelekea uchumi wa kisasa unaonufaisha wengi, bila ya shaka sekta binafsi itapaswa kuendelezwa kwa kulelewa na kujengewa uwezo zaidi na kuendelea kuwa mdau muhimu katika uchumi wa nchi yetu. Na kwa kuwa Chama cha Mapinduzi kina ujuzi na uzoefu mkubwa katika kuyajenga na kuyasimamia mazingira ya aina hiyo, sasa naomba nyote mkubaliane nami kuwa rais wetu ajae atoke CCM. Mhe. Spika, hili lilikuwa ni ombi haikuwa amri na ninaamini niliowaomba ni wastaarabu na waungwana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi ni chombo muhimu sana katika uongozi na mustakbali wa nchi yetu. Pia ni sehemu ya ukuzaji wa demokrasia nchini na ni taasisi yenye uzito mkubwa katika ustawi wa jamii na uchumi. Katika kuliwezesha Baraza hili serikali yangu imefanikiwa kama nilivyosema awali pale kulijenga jengo hili jipya.

Sasa napenda nishukuru kwanza kwa niaba yenu nyote, nimshukuru sana mfadhili mkubwa wa ujenzi huu Sheikh Abdulla Moh'd Al Youseif ambaye ametoa nusu ya gharama ya ujenzi wa jengo hili na nusu yake tumelipia sisi wenyewe. Kwa hivyo, sasa Baraza linajivunia kuwa na jengo lake wenyewe la kisasa na la kuvutia likiwa ni moja ya alama ya mhimili wa utungaji sheria. Nina imani kwamba Baraza litaendelea kutimiza wajibu wake kwa umahiri na ustadi mkubwa kwa faida ya kila mmoja wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hakuna marefu yasiyo na mwisho. Kipindi cha miaka mitano cha uhai wa Baraza hili kirefu lakini sasa kimefikia mwisho. Nachukua fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wote wa Baraza hili kwa kazi kubwa na nzuri ambayo mmeifanya wakati wote wa uhai wa Baraza lenu. *(Makofi)*

Mafanikio yote niliyoyataja hapo kabla yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na ushauri na maelekezo yenu na hata kuikosoa kwenu serikali. Pongezi za pekee ni zako wewe Mhe. Spika, Naibu wako na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza, Wajumbe wa Baraza na Katibu wa Baraza kwa uongozi mzuri wa shughuli za Baraza, kwa busara wakati wa vikao na kwa ufanisi mkubwa wa kuiendesha taasisi hii muhimu. *(Makofi)*

Sasa ninajua kwamba wengi wa wajumbe wako wamerudi tena majimboni kwenda kuomba ridhaa ya wananchi wawachague tena kuwa wawakilishi wao katika Baraza lijalo litakaloundwa baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 31. Nakuombeeni nyote kheri na mafanikio katika uchaguzi huo. *(Makofi)*

Kabla sijafanya ile kazi ya Kikatiba ya pili Mhe. Spika, nataka nirejee tena kukushukuru wewe na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili. Nawashukuru kwa *suprise* mliyonipa leo, ya zawadi ya ile hati maalum. Najua wazo lile limetokana na mshikamano uliomo ndani ya Baraza hili. Kwangu mimi nataka niseme ni faraja kubwa, maana sikutegemea kama nitapata zawadi kama ile. Zawadi ambayo nataka niwahakikishie kwamba nitaitunza na nitaienzi, nasema ahsanteni sana.

Mhe. Spika, mwisho kabisa. Kwa mujibu wa kifungu cha 92 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Maisha ya Baraza la Wawakilishi yataendelea kwa muda wa miaka mitano baada ya kuundwa upya mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu. Sasa ili kutoa nafasi ya matayarisho ya mwisho kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu ifikapo tarehe 31 Oktoba 2010, kwa madaraka niliyonayo chini ya kifungu cha 91(2)(a) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, natamka kwamba kuanzia Ijumaa tarehe 13 mwezi wa Agosti 2010 Baraza la Saba la Wawakilishi la Zanzibar litakuwa limevunjwa rasmi.

Nakutakieni Waheshimiwa Wajumbe na wananchi nyote saumu njema na Ramadhani ya baraka na wingi wa rehema.

Mwenyezi Mungu awabariki wote,
Mwenyezi Mungu Ibariki Zanzibar,
Mwenyezi Mungu Ibariki Tanzania,
Mwenyezi Mungu Ibariki Afrika.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Baraza ndio limeshavunjwa. Kazi iliyobaki hapa tuondoke kwa utaratibu na bahati nzuri Mhe. Rais hatuna deni. Lakini nataka niseme maneno mawili.

Mhe. Rais katika hotuba yako umezungumzia jambo la kihistoria la maamuzi ya wananchi na hatimaye kuwekwa kisheria na Baraza hili juu ya suala zima la Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Jambo hili ni la kihistoria, na kutambua hivyo sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tumeamua historia hiyo tuitunze. Historia hiyo tutaitunza kwa kutayarisha jiwe la kumbukumbu ambalo litakuwa na majina yote ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili la Saba. *(Makofi).*

Jiwe hilo litawekwa katika sehemu fulani maalum, ili iwe ni kumbukumbu Mhe. Rais kwa Baraza lako hili, kwa kazi kubwa ambayo tumeshirikiana na wewe pamoja na wananchi, ili kuleta mfumo mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Umoja wa Kitaifa. *(Makofi).*

Jiwe hilo atatutengenezea Mfadhili wetu Sheikh Abdalla Mohammed Al Yusouf, amekubali kufanya kazi hiyo. Mhe. Rais tunakushukuru sana kwa hotuba yako yenye nasaha nyingi na maneno ya hekima mengi. Nakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa watulivu kwa muda wote wakati Mhe. Rais anaendelea na hotuba yake.

Nawapongeza pia wageni wetu mbali mbali waliopo pale juu, nao wamekuwa watulivu na makini kabisa kumsikiliza Mhe. Rais wakati anatoa hotuba yake. Sasa mimi sina la kusema zaidi ya hapa, isipokuwa niseme kwamba mara baada ya kuondoka humu ndani tutakuwa na picha ya pamoja hapo nje, ambayo itawahusu Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na Mhe. Rais, bila shaka na ndugu yetu Mhe. Jaji wa Mahakama Kuu ambaye yupo hapa kwa niaba ya Jaji Mkuu wa Zanzibar.

Kwa hivyo, baada ya hayo machache naomba Waheshimiwa Wajumbe mbaki kimya, mara baada ya maneno haya nitawaomba tusimame sote kwa ajili ya wimbo wa taifa.

(Wimbo wa TaifaUlipigwa)

(Tarehe 11/08/2010 Saa 12:34 jioni Mhe. Rais alitamka kwamba kuanzia tarehe13/08/2010 Baraza la Saba la Wawakilishi litakuwa limevunjwa rasmi)